**Wafanyabiashara** Kariakoo wapewa siku 90 kuhama nyumba za NHC
UKURASA 5



**ACT-**Wazalendo yaja na mbinu za kuungana kupata katiba mpya
UKURASA 17


ama
ALHAMISI JUNI 15, 2023
AFYA NA MAZINGIRA
Ukurasa 12
Wadau na serikali wakaa pamoja kutathmini hali ya Ukimwi kitaifa
HARAKATI ZA MAZINGIRA NCHINI... Yalivyo mapambano kudhibiti uchafu uliosheni kwenye fukwe zilizoko nchini
Ukurasa 13
**Mpango MAMM uliobuniwa awamu ya nne, Rais aunoa kuboreshea afya ya leo**
• Mapya zahanati, hadi Muhimbili na pacha zake
Na Mwandishi Wetu

UKURASA 11

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Alhamisi Juni 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581342
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Kilichojificha wanafunzi kukwepa kidato cha tano

• **Wazazi**, wasomi waanika sababu zinazoshtua... *Endelea ukurasa 4*






Mwonekano wa Daraja lenye urefu wa kilomita 3 la JP Magufuli (Kigongo-Busisi), linalounganisha wilaya za Misungwi na Sengerema mkoani Mwanza jana, ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2024. **Picha nyingine:** Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wakazi wa mkoa huo, baada ya kukagua meli mpya ya abiria na mizigo ya MV Mwanza, inayoendelea kujengwa katika Bandari ya Mwanza South. **PICHA: IKULU**

## Samia aagiza TANROADS iwe na miradi bora nchini

UKURASA 2

BAJETI YA SERIKALI LEO

UKURASA 2

# Mwigulu kuja na hoja tano mpya

**MICHEZO** **NABI ATAJA MAENEO YA MABADILIKO YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikata keki jijini Dar es Salaam juzi, kuashiria kuanza kwa utekelezaji wa mpango kazi wa miaka mitano wa Shirika la Wateraid Tanzania (2023-2028) na Maadhimisho ya Miaka 40 ya shirika hilo hapa nchini. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kushoto), Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto), Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Hassan Kaduara (kulia) na Mkurugenzi Mkazi wa Water Aid Tanzania, Anna Tenga Mzinga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri Mwigulu kuja na hoja tano za kibajeti bungeni leo

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

MACHO na masikio ya watanzania leo yanatarajiwa kuelekezwa bungeni kushuhudia mikakati ya kibajeti ambayo serikali inakuja nayo kwa mwaka ujao wa fedha.

Bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/24 itakayowasilishwa bungeni jijini hapa baadaye leo na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, itatoa mwelekeo wa masuala ya kikodi na taswira ya gharama za bidhaa nchini.

Yanaporejewa mapendekezo ya ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, kuna hoja tano inatarajiwa kuja nazo, ikitarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 44.38 ikiwa ni ongezeko la asilimia saba kulinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/23 ya Sh. trilioni 41.48.

Serikali inatarajiwa kujikita katika kugharamia ajira za watumishi wapya wa umma, hasa wa sekta za afya na elimu, kugharamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu 2025.

Pia inatarajiwa kujielekeza katika kugharamia miradi ya kielelezo inayoendelea na kuja na utaratibu wa mpya wa utoaji wa mikopo kwa makundi maalum, inayotolewa kwa kukata asilimia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Ni bajeti ambayo Dk. Mwigulu alishaahidi itakuwa ya kubana matumizi kwa viongozi wa umma kwa kupunguza ununuzi wa magari, kufanya mikutano na vikao kwa njia ya mtandao.

**WAFANYABIASHARA**

Katika mazungumzo na Nipashe juzi, Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo, Martin Mbwana, alisema wanatarajia kuona serikali inapunguza kodi kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA), ili wafanyabiashara wamudu kushindana na nchi nane zinazowazunguka.



"Kwa mfano, biashara ya vitenge kwa kweli tumepigwa bao na wenzetu wa nchi za jirani kama vile Malawi, na ni kwa sababu wenzetu huko gharama za kuingiza mizigo bandarini ni ndogo sana kulinganisha na hapa kwetu. Tunaisikiliza serikali kwa kweli, iangalie namna ya kulitatua hili kupitia bajeti," alisema.

Mfanyabiashara wa nguo za kike katika Soko la Kariakoo, Anneth Mushi alisema anategemea bajeti hiyo kutoa ufumbuzi kuhusu kadhia ya uhaba wa dola ya Marekani. Kwa sasa kuna ugumu kuagiza mizigo nje ya nchi, hasa China.

**SEKTA USAFIRISHAJI**

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Maroli Wadogo na wa Kati (TAMSTOA), Chuki Shabani, alisema wanatarajia kuona serikali inapunguza kodi wanayotakiwa kuilipa kabla hawajapata faida (advance tax) ili kuokoa sekta ya usafirishaji nchini.

Alisema kodi hiyo katika mwaka wa fedha 2022/23 inatozwa Sh. milioni 2.790 kwa kila lori, jambo analolilalamikia limesababisha baadhi ya wamiliki kushindwa kulipa na kupendekeza iwe Sh. milioni moja kwa mwaka.

**WAFANYAKAZI**

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Paul Loisulie, alisema matarajio ya watanzania na wafanyakazi ni serikali kuna na bajeti itakayopunguza gharama za maisha.

"Bajeti ikija na sera nzuri, labda ya kuweka ruzuku katika mafuta, itarahisisha vitu na kuleta unafuu wa maisha.

"Wafanyakazi tunatarajia bajeti hii itukumbuke, tumeachwa nje ya bajeti kwa miaka mingi. Kama Rais alivyotuahidi nyongeza ya kila mwaka, ikitekelezwa itakuwa ni kitu kikubwa kwa wafanyakazi na watanzania," alisema.

**WABUNGE**

Mbunge wa Tabora Kaskazini (CCM), Almas Maige, alisema anatarajia bajeti hiyo itashusha neema maeneo ya vijijini kwa kutekelezwa miradi ya maendeleo.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema ni vyema serikali ikazingatia maoni ya wabunge na ushauri kuhakikisha inabana matumizi, ili kutoacha makovu kwa wananchi.

"Ni vizuri yale malalamiko ya utitiri wa tozo serikali iyafanyie kazi na vyanzo visivyo vya uhakika vinavyosababisha makovu kwa wananchi kama tozo za simu ziangaliwe," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, alisema katika bajeti hiyo matumaini yaliyopo ni serikali kuzingatia mahitaji ya wananchi katika miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alisema serikali inapaswa kufanyika kazi kilio cha utitiri wa tozo kwa wananchi kinachosababisha watu wasilipe kodi kwa hiari.

Mkazi wa Dodoma, Mark Masudi, alishauri bajeti izingatie vipaumbele vinavyogusa wananchi wa hali ya chini na kusisitiza fedha zinazotengwa zifike kwenye maeneo husika.

Aliomba kodi zinazowekwa ziwe rafiki kwa wananchi badala ya kuwa kikwazo ili kuwafanya watanzania walipe kodi kwa hiari.

***Imeandaliwa na Augusta Njoji na Jenifer Gilla**

# Samia aagiza TANROADS iwe na miradi bora iliyokaguliwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kusimamia upimaji wa ubora wa miradi inayotekelezwa, ukiwamo wa ujenzi wa Daraja la JPM (Kigongo-Busisi).

Ameonya kuwa tabia za kuliacha jukumu hilo kwa makandarasi wageni ni hatari kwa kuwa kuna uwezekano wa kutekelezwa miradi isiyo na ubora.

Mkuu wa Nchi alielekeza hayo jana alipokagua mradi ujenzi wa Daraja la JPM (Kigongo-Busisi). Alisema ni lazima TANROADS wahakikishe wanafanya majaribio katika miradi na kujihakikishia ni imara, inakidhi vigezo na yenye tija kwa wananchi.

"Hawa makandarasi na ndugu zetu ni wa kupita tu na hii ni mali yetu sisi na vizazi vyetu. Kwa hiyo hakikisha mnatumia vipimo vya ndani zikiwamo maabara ili kujihakikishia ubora wake. Isije kutokea daraja kama hili linaanza kuporomoka na kutuzamisha majini, zingatieni hilo," aliagiza.

Rais Samia pia aliwataka wananchi kuwa sehemu ya usimamizi wa mradi huo na kuacha tabia za udokozi wa vifaa. Wampe nafasi mkandarasi na wataalamu wake kukamilisha mradi mapema.

**Hawa makandarasi na ndugu zetu ni wa kupita tu na hii ni mali yetu sisi na vizazi vyetu. Kwa hiyo hakikisha mnatumia vipimo vya ndani zikiwamo maabara ili kujihakikishia ubora wake. Isije kutokea daraja kama hili linaanza kuporomoka na kutuzamisha majini, zingatieni hilo.**

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wa kielelezo, Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mohamed Besta, alisema una urefu wa kilometa tatu kwa upande wa daraja na barabara unganishi kilometa 1.6.

Alibainisha kuwa kwa pamoja umefikia asilimia 75, ikiwa ni nyuma ya matarajio. Kwa mujibu wa mpango kazi, mradi huo kwa sasa ulitakiwa kuwa umefikia asilimia 89.

Alitaja sababu za kuchelewa kukamilika kwa mradi huo zinajumuisha kuongezeka kwa kina cha maji, maradhi ya UVIKO-19 na utofauti wa jiolojia katika miamba iliyomo ziwani.

Alisema mradi huo wenye gharama ya Sh. bilioni 706.33 ulioanza kutekelezwa Februari 25, 2020, unatarajiwa kukamilika mwezi Februari mwakani na mkandarasi tayari amelipwa zaidi ya Sh. bilioni 368.6. Pia Sh. bilioni tatu zimetumika kuwalipa fidia wananchi huku Mhandisi Mshauri akilipwa Sh. bilioni nne.

Katika ziara yake hiyo ya siku tatu mkoani Mwanza, Rais Samia pia alitembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa meli kubwa ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 82. Alieleza kuridhishwa na mradi huo.

"Ningesimama tu na kuwaambia zalisheni mngeniuliza 'tutauza wapi?' Sasa niwahakikishie kuwa chochote kitakachozalishwa nchini lazima kipelekwe sokoni na kazi hii inafanyika pia katika mikoa yote yenye bandari nchini," alisema.

Rais Samia aliahidi kurejea mkoani Mwanza ndani ya miezi miwili ya ukamilishwaji wa meli hiyo kubwa ili awe wa kwanza kuizindua kwa kuipanda na kuzunguka nayo ndani ya ziwa hilo.



Katika ziara hiyo Rais Samia, baada ya kuwasili Sengerema, alishuka katika gari na kwenda kumsalimia, Juliana Kidaso ambaye ni Mama Mkwe wa Rais wa Awamu ya Nne, Hayati Dk. John Magufuli, aliyekuwa ameketi katika moja ya mahema.

Baada ya mazungumzo ambayo yalichukua dakika kadhaa, Juliana ambaye ni mama mzazi wa Janeth Magufuli, alionekana akimwombea Rais Samia.

## HABARI KITAIFA



Mchuuzi wa samaki (kushoto), akisubiri wateja katika soko la Bagamoyo, mkoani Pwani jana. Kutokana na kuanza kwa kipindi cha baridi samaki wamekuwa hawapatikani kwa wingi na kusababisha fungu moja kuuzwa kwa bei ya 7,000/- hadi 8,000/-. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wadau wachekelea ma-DED kuzuiwa kusimamia uchaguzi

**Na Sabato Kasika**

WADAU wa haki za binadamu wameeleza kufurahishwa na hukumu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kuiamuru serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, wakidai kilio chao kimesikika.

Mdau wa haki za binadamu, Bob Wangwe kwa kushirikiana na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), walifungua kesi Na. 011/2020 dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kesi hiyo ilikuwa inapinga kifungu cha 6(1), 7(1), 7(2) na 7(3) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ambavyo vinaruhusu wakurugenzi wa halmashauri (ma-DED) kusimamia uchaguzi nchini.

Mahakama hiyo ilitoa uamuzi juzi kwamba Kifungu cha 6(1), 7(1) na 7(3) vya sheria hiyo vinakiuka Ibara ya 13(1) ya Mkataba wa Afrika ambao unatoa haki ya kila mtu kushiriki katika uongozi wa nchi kwa kuchaguliwa au kupitia wawakilishi kwa mujibu wa sheria.

Akizungumzia hukumu hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema jana kuwa ni vyema sasa serikali ikapeleka haraka bungeni muswada wa kubadilisha sheria ya uchaguzi.

"Inaweza kuupeleka Septemba mwaka huu au Januari mwaka ujao, ufanyiwe kazi haraka kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa ili wasimamizi wawe wale ambao hawana chembe ya ukada wa chama chochote," alisema Dk. Anna.

Alisisitiza kuwa hukumu hiyo ni ushindi wa wapenda haki za binadamu na hata wapenda demokrasia, kwa maelezo kwamba kumekuwa na upendeleo wakurugenzi wanaposimamia uchaguzi.

Alisema umefika wakati sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa na maofisa wao wa kusimamia uchaguzi badala ya kutegemea wakurugenzi wa halmashauri, ambao wengi wao ni makada wa vyama vya siasa.

"Tuliwahi kufanya utafiti nchi nzima mwaka 2015 na kuangalia utendaji wa wakurugenzi na kubaini kuwa wengi wao ni makada wanaoshindwa katika kura za maoni na kuteuliwa kushika nafasi hiyo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kada wa chama hawezi kukubali chama chake kishindwe. Atafanya kila njia kuhakikisha kinashinda. Ni mazingira yanayominya haki na demokrasia.

Mwanasheria na Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, alisema uamuzi huo ni hatua nzuri ambayo ni mwelekeo wa kufikia demokrasia ya kweli.

"Kilichofanyika si haba, ni mwendelezo wa kutafuta demokrasia, kwani haba na haba hujaza kibaba, hivyo kila sehemu ambayo tutaona kuna tobo, tutaendelea kuifanyia kazi," alisema Bob.

Kesi hiyo ilifunguliwa baada ya Mahakama ya Rufani kutoa uamuzi kwamba kifungu hicho hakikiuki Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika rufani namba 175 ya mwaka 2020 katika shauri la Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Dickson Sanga.

# Watumishi wafukuzwa kazi ubadhirifu fedha za umma

**Na Moses Ng'wat**, TUNDUMA

WATUMISHI sita katika Halmashauri ya Mji Tunduma wilayani Momba wamefukuzwa kazi na wengine wawili kupewa adhabu ya kukatwa asilimia 15 ya mishahara yao kwa kipindi cha miaka mitatu baada ya kupatikana na makosa mbalimbali yakiwamo ya ubadhirifu.

Halmashauri hiyo pia imemshusha wadhifa Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Halmashauri hiyo, Ronald Msangi, huku watumishi wengine wanne wakinusurika baada ya uchunguzi kubaini hawana hatia katika makosa yaliyokuwa yanawakabili.

Uamuzi huo ulifikiwa mwishoni mwa wiki na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo katika kikao cha baraza maalum lilipogeuka kuwa kamati kwa lengo la kupitia na kujadili mashauri mbalimbali ya kinidhamu yaliyowasilishwa katika kikao hicho, yakiwamo ya ubadhirifu.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ayoub Mlimba aliwaambia wandishi wa habari kuwa baraza lilifikia uamuzi huo kufuatia hoja zilizoibuliwa na madiwani katika baraza mwezi Desemba mwaka jana.

"Baraza tumejigeuza kama kamati kwa mujibu wa sheria na kanuni tulizonazo ili kupitia mashauri mbalimbali ya watumishi waliofanya vibaya katika nafasi za utumishi wao.

Mlimba alisema watumishi hao waliochukuliwa hatua walikuwa wamegawanyika katika makundi mawili - watumishi wa halmashauri walio katika ajira za kudumu na wale wa ajira za mkataba.

Aliwataja watumishi wa ajira za kudumu waliofukuzwa kuwa ni Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi cha halmashauri hiyo, Obeid Mwakalinga, Ofisa Ununuzi Daraja la Pili, Ibrahim Lulimo, Mhandisi Daraja la Pili, Aly Farayo, na Dickson Kisemine ambaye ni Mhandisi Daraja la Pili.

Aliwataja watumishi wengine wawili waliofukuzwa kazi ambao walikuwa katika ajira za mkataba katika halmashauri hiyo ni Ally Hassan ambaye alikuwa Mhandisi wa Majengo na Japhet Chota aliyekuwa Mhadisi Ukadiriaji Majenzi.

Mlimba alisema katika kikao hicho, watumishi wawili ambao ni Patricia Mbigili, Ofisa Elimu Sekondari wa halmashauri na Raphael Simkonda, Ofisa Mtendaji Daraja la Tatu wamepewa adhabu ya kukatwa asilimia 15 ya mishahara yao kwa kipindi cha miaka mitatu.

Baraza hilo pia limetoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo ya Mji Tunduma, Philemon Magesa kuhakikisha kabla ya kuwarudisha kazini watumishi ambao hawakukutwa na hatia, wakiwamo waliopewa adhabu ya kukatwa mishahara yao, lazima aandae kikao cha pamoja kati ya watumishi hao na kamati ya fedha ili kuwekana sawa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

eGA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini "Office Chairs", "Printers" na "Laptops" na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
"Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma"

# Kilichojificha wanafunzi kukwepa kujiunga kidato cha tano na sita

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

BAADHI ya wasomi, wazazi na wadau wa elimu nchini wameeleza mtazamo wao kuhusu wimbi la sasa la wahitimu wengi wa kidato cha nne, kuachana na masomo ya kidato cha tano na kutimkia vyuo vya kati kusomea fani mbalimbali.

Akizungumzia wimbi hilo, Mkufunzi na Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii ya TICD-Tengeru, Adrian Lyapembile, alisema wanafunzi wengi wanafanya hivyo kwa kuwa wanaona vyuo vya kati vitawasogeza haraka kupata ujuzi na ajira, badala ya kupoteza muda wa miaka miwili sekondari, na wakihitimu watalazimika kusoma tena diploma miaka miwili.

"Wazazi wengi na hata wanafunzi wenyewe wanaamini shule ile ya miaka miwili ya kidato cha tano na cha sita ni kama wanakwenda kupoteza muda, kwa sababu ile miaka miwili akimaliza anarudi bila ujuzi wowote.

"Kwa hiyo, wengi wanapendelea mtoto aende vyuo vya kati, akasomee ujuzi ambao atarudi nao na utamsaidia kupata ajira au kujiari mwenyewe. Ndiyo! miaka miwili atakuwa amesoma NTA Level 4 na NTA Level 5, ambayo ni ngazi ya cheti na akiongeza mwaka wa tatu anapata Diploma.

"Inaonekana ni rahisi zaidi kwa sababu huyo aliyesoma kidato cha tano na sita, bado atahitaji tena kusoma miaka miwili ya kupata diploma," alifafanua.

Sia Lyimo, Mkazi wa Kijenge jijini Arusha, alisema kwa sasa wazazi/walezi wengi wanawapeleka watoto wao kujiunga na vyuo vya kati kwa kuwa vinawasaidia kuongeza ujuzi unaowapa fursa ya kujiajiri au kuajiriwa mapema, badala ya njia ndefu ya kupita kidato cha tano na sita.

"Wazazi wengi, nikiwamo mimi tunafanya hivyo kama njia mojawapo ya kutua mzigo wa kuwa na mwanafunzi anakaa darasani muda mrefu pasipo kupata ujuzi wa aina yoyote.

"Vyuo vya ufundi, vina uwanda mpana wa mwanafunzi wa kutengeneza ajira nyingi na kutatua tatizo la ajira kwa sababu mwanafunzi atapata ujuzi wa kufanya mambo muhimu kwa vitendo badala ya nadharia.

"Unakuta mwanafunzi anahitimu elimu ya chuo kikuu lakini akija mtaani, hawezi kufanya kazi ya aina yoyote itakayomwingizia kipato. Lakini kwa waliosoma elimu ya vyuo vya ufundi mwenye (astashahada na stashahada), wana ujuzi wa kupata ajira au kujiajiri," alisema.

Mkufunzi wa kujitegemea ambaye pia aliwahi kufundisha Chuo cha Ualimu Marangu, Patrick Mwiya, alisema sasa ajira inaonekana ni tatizo kubwa na vijana wanataka kuanza maisha mapema.

"Mathalani, kijana huyu amepata daraja la kwanza, daraja la pili au la tatu, anaona ni vyema apate ujuzi, maana waliomaliza vyuo vikuu wako mtaani. Hawana ajira! Hivyo, wanaona haina maana.

"Wanatafuta kozi inayoendana na maisha halisi, na ndio maana hata serikali hivi sasa imeanza kufanya mapitio ya mitaala ya elimu yetu ili kuendana na hali halisi ya maisha ya sasa," alisema Mwiya.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Dk. Easther Towo, alisema sababu kubwa inayochagiza vijana wengi kuacha kwenda kusoma ngazi hiyo ya sekondari ni urefu wa kufikia ujuzi na ajira.

"Yaani hiki kitu hata mimi kinanichanganya, Nina kijana wa mama mmoja, anatusaidia pale nyumbani. Amekataa katakata kwenda kidato cha tano na amepata daraja la pili. Ameng'ang'ania hataki. Anasema anataka akajifunze masuala ya mifugo.

"Ninadhani kuna haja vyuo vikuu vifanye utafiti wa kina, ili kupata kiini cha haya yote. Wengine wanasema wanawaona hawa waliomaliza kidato cha sita wako mtaani wanasubiri kujiunga na vyuo, wengine wanapambana kutafuta ajira na wametumia muda mrefu kusoma bila kuyafikia mafanikio," alisema.

Juni 11 mwka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angelah Kairuki, wakati anatangaza majina ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo, alisema wanafunzi 129,830 (wasichana 66,343 na wavulana 63,487) sawa na asilimia 69 ya wenye sifa, wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za kidato cha tano 540, zikiwamo shule mpya 29 zinazotarajiwa kuanza kutoa huduma mwaka huu.

Waziri huyo alisema wanafunzi 1,878 (wasichana 1,097 na wavulana 781) wamepangiwa katika shule za sekondari maalum nane; Kilakala, Mzumbe, Ilboru, Kisimiri, Msalato, Kibaha, Tabora Boys na Tabora Girls.




Kamishna wa Elimu wa Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, Dk. Lyabwene Mutahaba (kushoto), akipata maelekezo kutoka kwa Mwanzilishi Mwenza wa SILABU, Adam Duma (kulia), kuhusu namna aplikesheni ya SILABU inavyofanya kazi katika uzinduzi wake, jijini Dar es Salaam jana, itakayowawezesha wanafunzi na watanzania kujifunza mtandaoni. Wengine ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Huduma kwa Wateja wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Harriett Lwakatare (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Huduma za Kidigitali wa kampuni hiyo, Nguvu Kamando. Habari Uk. 19. **NA MPIGAPICHA WETU**

# TNMC yalaani muuguzi kumbaka mjamzito

**Na Beatrice Shayo**

BARAZA la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) limelaani vikali kitendo cha kinyama na ukatili uliopitiliza kinachodaiwa kufanywa na Muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, Rayson Duwe, kumbaka mjamzito.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Juni 9 mwaka huu saa mbili usiku, muuguzi huyo aliyekuwa zamu, akituhumiwa kwenda chumba cha wagonjwa na kumbaka mama huyo ambaye anakaribia kujifungua. Alikuwa anapatiwa matibabu ya ugonjwa wa malaria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi kwa vyombo vya habari na kutiwa saini na Msajili wa TNMC, Agnes Mtawa, baraza limesikitishwa na kitendo hicho na kuwataka wauguzi kufuata maadili ya kazi.

"Baraza lilipata taarifa ya Muuguzi Msajili wa Baraza anayetuhumiwa kumbaka mjamzito aliyefika hospitalini kwa ajili ya kupata matibabu. Baraza linalaani kitendo hicho ambacho ni cha kinyama, ukatili uliopitiliza na ni kinyume cha maadili ya uuguzo na ukunga.

"Baraza linatoa pole kwa mama aliyepata madhila hayo. Baraza linaujulisha umma kuwa baada ya taratibu za uchunguzi na vyombo vya sheria kuthibitisha muuguzi huyo kutenda kitendo hicho, litachukua hatua za kinidhamu na kitaaluma kwa mujibu wa kifungu cha (25)(2) (c) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010," baraza hilo lilieleza katika taarifa yake hiyo.

Baraza hilo pia limetoa wito kwa wauguzi na wakunga nchini kutoa huduma kwa kuzingatia utu, taratibu, kanuni na sheria.

"Kwa matendo kama haya yanaaibisha taaluma ya wauguzi ambao ni kiungo katika upatikanaji wa huduma bora za matibabu," lilionya.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Baraza la Ukunga ni mamlaka ya kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya usimamizi wa taaluma na wanataaluma ya uuguzi na ukunga nchini.

# Mkuu wa Majeshi ataka ubunifu wa miradi JKT

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, ameitaka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wakati likijiandaa kuadhimisha miaka 60, lijitathmini kubuni miradi mikubwa ya kimkakati itakayoendana na Dira ya Taifa.

Aliagiza hayo juzi Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kituo cha mafuta cha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kilichojengwa maeneo ya Mlalakuwa, kikiwa ni miongoni mwa miradi inayofanywa na shirika hilo.

Kituo hicho ambacho kinajulikana kama SUMAJKT Energies ni miongoni mwa vituo vya mafuta ambavyo shirika limepanga kuvijenga kwenye majiji yakiwamo Arusha, Dodoma, Mbeya na Tanga.

"Julai Mosi mwaka huu, JKT litaadhimisha miaka 60. Hiki ni kipindi kirefu, na jeshi limefanya mambo mengi na makubwa. Mradi wa kituo hiki cha mafuta ni mojawapo ya miradi mingi ya JKT chini ya SUMAJKT.

"Miradi ndiyo namna sahihi ya kuongeza uwezo wa kujitegemea, ni darasa muhimu kwa vijana ili kuwafanya wawe wabunifu na kuwa na uzoefu wa kuiendesha. Inawaandaa vijana kujitegemea na kuwa na kuongeza kiwango cha uzalendo wa kuilinda nchi," alisema.

Kiongozi huyo alisema wakati wakielekea miaka 60, anaamini umefika wakati kuanza kubuni miradi mikubwa ya kimkakati ambayo lengo lake litakuwa ni kuimarisha ulinzi wa nchi.

"Tufikirie kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati itakayoendana na Dira ya Taifa. Ninatambua Jeshi la Kujenga Taifa ndio kazi yenu, mmekuwa mkifanya miradi mingi, nina wanawaasa mfanye miradi mingine mikubwa zaidi," aliagiza.

Aliwataka waendelee kuanzisha vituo vya mafuta kila mahali kwa kuwa SUMAJKT ndiyo kinara wa kubuni miradi.

Mkuu wa JKT, Jenerali Rajab Mabele alisema kituo hicho ni moja ya maelekezo yake na wamejipanga wawe na vituo kama hivyo katika majiji yote.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Kanali Petro Ngata, alisema shirika kwa kutambua malengo ya kuanzishwa kwake, ambayo ni kuchangia uwezeshaji wa shughuli za JKT na kujenga uchumi wa taifa, limeamua kuwekeza kwa kujenga kituo hicho cha mafuta.

# Airtel wachangia damu kuboresha huduma afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI Kampuni ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Uchangiaji Damu nchini (NBTS) jana wamechangia damu kwa hiari ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha afya nchini.

Siku ya Damu Salama hutumiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhamasisha afya salama. Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Give blood, give plasma, share life, share often' kudhihirisha umuhimu wa kila mtu kujitoa kwa zawadi ya kipekee kwa kuchangia damu na kuokoa maisha ya wahitaji.

Mkurugenzi Rasimali watu Airtel, Stella Kibacha, alisema kuchangia damu ni jambo muhimu linalosaidia kuokoa maisha ya wenye uhitaji. "Tunatambua kwamba damu inahitajika sana hospitali na hasa pale kinamama wanapokuwa wanajifungua, vile vile, kwa watoto wenye magonjwa mbali mbali, kama malaria, majeruhi wa ajali, wagonjwa wa kansa pamoja na wagonjwa wengine.

"Kwa sababu hiyo, sisi wafanyakazi wa Airtel tumeamua kuchangia damu na pia tukio hili liwe hamasa kwa wananchi wengine kijitokeza na kuchangia," alisema Kibacha.

Msimamizi wa uchangiaji damu wa Kanda ya Kati, Fatma Majungu alisema, Benki ya damu salama nchini inahitaji uniti za damu 600,000 kwa mwaka kwa ajili ya huduma za dharura na matumizi mengine ya afya, lakini makusanyo ya damu kwa mwaka jana ni asilimia 65 ya mahitaji ya benki hiyo.

"Upatikanaji wa damu bado ni changamoto. Taarifa ya mwaka 2019/2020 ya ukusanyaji wa damu nchini inaonyesha kuwa asilimia 60 ya waliochangia damu walifanya hivyo kwa hiari yao na kati yao ni asilimia nane pekee hufanya hivyo mara kwa mara. Bado tunahimiza wachangiaji kuendelea kuchangia kutokana na uhitaji wa damu tulionao," alisema Fatma.

"Naniwapongeza Watanzania pamoja na wafanyakazi wa Airtel kwa kujitokeza kushiriki kwenye zoezi hili la kuchangia damu kwa mwaka huu na niwaombe waendelee hivyo ili kuendelea kuokoa maisha ya wengine," aliongeza Fatma.

Siku ya kuchangia damu unaadhimisha Juni 14 kila mwaka. Siku hii ni maalum kukumbuka na kutambua umuhimu wa damu salama. Pia ni siku ya kusherehekea na kuwakumbuka wote wanaochangia damu kwa hiari.

**Kwa sababu hiyo, sisi wafanyakazi wa Airtel tumeamua kuchangia damu na pia tukio hili liwe hamasa kwa wananchi wengine kijitokeza na kuchangia.**

# Mpango kutoa elimu VVU kwa vijana waja

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU, Tanzania (NACOPHA) limekuja na mpango mpya wa kutoa elimu kwa vijana wa umri wa miaka 16 mpaka 25 ili kutambua njia sahihi za kujikinga na maambukizi.

Mpango huo pia unalenga kuwapatia ujasiri wale wenye maambukizi kujitokeza katika jamii.

Hayo yalibainishwa jana katika hafla iliyoandaliwa na NACOPHA kwa kushirikiana na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na Ukimwi (PEPFAR), ikishirikisha vijana wanaoishi na maambukizi hayo ili kutambua changamoto wanazozipitia katika jamii.

Akizungumza katika hafla hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NACOPHA, Deogratias Lutatwa, alisema dhamira yao kwa sasa ni kuhakikisha wanawafikia vijana kwa wingi kwa kuwapatia elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

"Tuna mpango wa kuwafikia vijana, hususani wale wenye umri kuanzia miaka 16 mpaka 26. Takwimu zinaonyesha kundi hili ndiyo huathirika kwa wingi, kutokana kutokuwa na elimu ya kutambua afya zao," alisema.

Aliongeza kuwa watahakikisha wanawafikia vijana wengi hata wale ambao wanaishi sehemu za vijijini.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Wanaoishi na VVU Tanzania (NYP+), Pudensiana Mbwiliza, alisema changamoto iliyopo ni vijana wengi kukosa ujasiri wa kueleza hali zao kutokana na hofu ya kutengwa na jamii.

Alisema vijana wengi hususani waliopo katika vyuo mbalimbali, wamekuwa wakichukulia ugonjwa huo ni wa kawaida, hali ambayo wamejikuta wakikumbana na tatizo hilo bila ya wao kutambua.

Mratibu wa UKIMWI Duniani wa PEPFAR, Balozi John Nkengason, aliipongeza Tanzania kwa kupiga hatua nzuri kufikia malengo ya Umoja wa Mataifa.

"Kwa kushirikiana pamoja tunapaswa kupinga maambukizi kuendelea, kwani utafiti unaonyesha watu wanaoishi na VVU hawajui afya zao," alisema.

Mratibu wa PEPFAR nchini, Jessica Green alisema watatekeleza programu zote ambazo zinakidhi mahitaji yao.

Wakati juhudi hizo zikifanyika, ripoti ya Utafiti wa matokeo ya UKIMWI Tanzania 2016-2017 inaonyesha maambukizi ya VVU yanapungua kadri ya ngazi ya elimu ya vijana ilivyo (kutoka shule ya msingi hadi sekondari).

Ripoti inaonyesha Tanzania ina watu wanaoishi na VVU takribani milioni 1.4 huku wasichana wakitajwa kuwa na maambukizi ya VVU kwa kiwango kikubwa kulinganishwa na wavulana.

Maambukizi ya UKIMWI kwa vijana wasio na elimu ni asilimia 6.1, huku wenye elimu yakiwa kwa asilimia 0.5.



Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashim Komba akipanda mti wakati akizindua kampeni ya "Mti Wangu Tanzania Yangu", Dar es Salaam juzi, yenye lengo la kulinda mazingira. Miti 10,000 inatarajiwa kupandwa katika wilaya hiyo kwa Mwaka 2023/24. **PICHA: MARIAM MKANANKA**

# NHC yatoa siku 90 wakazi Kariakoo kupisha nyumba

**Na Halfani Chusi**

WAKAZI na wafanyabiashara zaidi ya 1,000 wamepewa notisi ya miezi mitatu kuhama katika majengo ya Kariakoo yanayomilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Imeelezwa kuwa notisi hiyo inatokana na mpango wa serikali kuingia ubia na mwekezaji kuboresha nyumba hizo, hali iliyoibua malalamiko kutoka kwa wakazi na wafanyabiashara hao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na shirika hilo, na Meneja wa Mkoa, Nistas Mvungi, uamuzi huo umetokana na shirika kurejea kipengele namba 4:1 (C) (d) na 7.2 cha mkataba wa upangaji kinachompa mamlaka kuvunja mkataba ndani ya siku 90 pale anapohitaji jengo lake kwa ajili ya matumizi mengine.

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kuwa kwa maelezo hayo, wakazi wanapewa notisi ya siku 90 ya kutakiwa kuhama katika nyumba wanazoishi, ili kupisha uendelezaji unaokusudiwa kufanyika.

Ilifafanuliwa zaidi katika taarifa hiyo kuwa wanapangaji wanaruhusiwa kuomba upangaji upya baada ya jengo jipya kukamilika kulingana na masharití ya kipindi hicho.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, alikiri kuwa na taarifa hiyo na alipanga kufanya kikao na wafanyabiashara wanaoishi katika nyumba hizo ili kuwa na kauli ya pamoja.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Muuguzi anayedaiwa kubaka ameidhalilisha taaluma

**KATI** ya matukio mabaya ambayo yameshatokea katika sekta ya uuguzi ni la muuguzi mmoja anayedaiwa kuvuka mipaka na kumfanyia ukatili mgonjwa wake kwa tuhuma za kumbaka.

Muuguzi huyo ambaye alikuwa msaidizi Daraja la II, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma hizo alizomfanyia mgonjwa ambaye ni mjamzito.

Mbinu anayodaiwa kutumia muuguzi huyo inaonesha wazi kuwa alidhamiria kufanya kitendo hicho kwa kuwa inadaiwa alitumia sindano ya usingizi kumdunga mgonjwa ili aweze kutimiza lengo lake.

Pia, kwa mujibu wa taarifa za jeshi la polisi, muuguzi huyo ambaye siku ya tukio alikuwa zamu, alikuwa eneo la mapokezi ya wagonjwa wa nje na aliingia kazini akiwa amelewa.

Kutokana na tuhuma zinazomkabili muuguzi huyo, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), limelaani vikali kitendo cha kinyama na ukatili uliopitiliza unaodaiwa kufanywa na muuguzi huyo wa Hospitali ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Juni 9, mwaka huu majira ya saa mbili usiku baada ya muuguzi huyo aliyekuwa zamu kutuhumiwa kwenda chumba cha wagonjwa wa ndani na kumbaka mama huyo ambaye alikuwa siku za karibu kujifungua na alikuwa akipatiwa matibabu ya ugonjwa wa malaria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Msajili wa TNMC, kitendo hicho kimewasikitisha na kuwataka wauguzi kufuata maadili ya kazi.

"Baraza lilipata taarifa ya Muuguzi Msajili wa Baraza anayetuhumiwa kumbaka mjamzito aliyefika hospitali hiyo kwa ajili ya kupata matibabu. Baraza linalaani kitendo hicho ambacho ni cha kinyama, ukatili uliopitiliza na ni kinyume na maadili ya uuguzi na ukunga."

Baraza hilo limetoa pole kwa mama aliyepata madhila hayo na kuujulisha umma baada ya taratibu za uchunguzi na vyombo vya sheria kuthibitisha muuguzi huyo kutenda kitendo hicho, Baraza litachukua hatua za kinidhamu za kitaaluma kwa mujibu wa kifungu cha (25) (2) (c) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Kadhalika kitendo anachotuhumiwa kufanya muuguzi huyo, kimelikumbusha Baraza kuwataka wauguzi na wakunga nchini kutoa huduma kwa kuzingatia utu, taratibu, kanuni na sheria.

Baraza hilo linasema matendo kama hayo yanaaibisha taaluma ya wauguzi ambao ni kiungo katika upatikanaji wa huduma bora za matibabu.

Kwa hakika kitendo anachotuhumiwa kufanya muuguzi huyo kimeidhalilisha sekta hiyo na kuwafanya wananchi kuingia hofu wanapokwenda kupata matibabu.

Muuguzi ni mtu anayeaminiwa ndiyo maana wagonjwa wanakuwa huru kueleza matatizo yao kwa uwazi wakiamini kuwa ni watu wenye maadili yanayozingatia taaluma zao.


Wagonjwa wakimbile wapi kama eneo wanalostahili kupata huduma sahihi, anatokea mtu mmoja na kulichafua?

Taarifa ya Baraza la Ukunga ni Mamlaka ya kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya usimamizi wa taaluma na wanataaluma ya uuguzi na ukunga nchini.

Lengo la kuanzishwa chombo hicho ni kuhakikisha jamii inapata huduma zilizo bora na salama kutoka kwa wauguzi na wakunga. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Imani hii potofu kwenye matumizi ya vyandarua, daima isipewe nafasi

Na Sabato Kasika

**KWA** muda mrefu kumekuwapo kampeni ya kuhamasisha jamii kutumia vyandarua vilivyowekewa dawa, ili kujikinga dhidi ya mbu wanaoweza kueneza ugonjwa wa malaria.

Lakini, pamoja na kampeni hizo, bado wapo baadhi ya watu ambao hawataki kuvitumia, badala yake vinageuzwa kuwa nyavu za kuvulia samaki au kuzungushia bustani za mboga zisiharibiwe na kuku.

Sababu kubwa ya kufanya hivyo, ni madai kwamba dawa zinazowekwa kwenye vyandarua hivyo zinaweza kuua nguvu za kiume. Ni madai ambayo katika ukweli, pia sababu za kitaalam, zinatokana na elimu ya mtaani.

Nadhani umefika wakati sasa jamii kuachana na imani hizo potofu, ili kukinga dhidi ya ugonjwa huo, ambao ni miongoni mwa magonjwa yanayoua watu wengi duniani.

Kaulimbiu katika maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani kwa mwaka huu, ilikuwa ni 'Dhibitini Maambukizi ya Malaria', huku takwimu zikionyesha mikoa inayoongoza kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria kuwa ni Tabora kwa asilimia 23 na Mtwara asilimia 20.

Mikoa mingine inatajwa; Kagera kwa asilimia 18, Shinyanga asilimia 16 na Mara na asilimia 15, huku mikoa tisa ya; Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Dodoma, Songwe, Iringa, Dar es Salaam na Mwanza, ikiwa ina kiwango cha maambukizi chini ya asilimia moja.

Takwimu hizo zilitolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati wa maadhimisho hayo hivi karibuni, na kwamba, serikali imedhamiria kutokomeza maambuzi ya ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Katika vita dhidi ya malaria, akasema serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya na kinga kama vyandarua vyenye dawa na upatikanaji wa vitendanishi na dawa za malaria.

Sasa kwa kuwa mkakati wa serikali ndiyo huo, basi jamii haina budi kuunga mkono juhudi hizo kwa kutumia vyandarua vyenye dawa za kuzuia mbu badala ya kuegemea kwenye imani potofu.

Binafsi, sidhani kwamba kuna serikali ambayo mikakati yake ni kuangamiza wananchi wake. Ninaamini kuwa, hadi wataalam wa afya wanaruhusu matumizi ya vyandurua hivyo, walishajiridhisha kuwa havina madhara kwa watumiaji.

Kuwapo kwa baadhi ya watu wanaoamini kuwa vinapunguza nguvu za kiume, kunatajwa ni sawa na kupingana na sayansi na kukumbatia mambo ya kuhisi badala ya kukubaliana na uhalisia.

Serikali inasema, maambukizi ya malaria yanaendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 8.1 mwaka 2022 kama alivyoeleza Waziri Mkuu, hivyo jamii kuendelea kujikinga na ugonjwa huo ni jambo la muhimu.

Takwimu hizo za serikali zinaonyesha malaria kupungua, sasa kwa nini baadhi ya watu wanapingana na matumizi ya vyandarua? Ninadhani watu hao wanatakiwa kusaidiwa wabadilishe mtazamo.

Ninaamini wapotoshaji wapo na wanaendelea kupotosha kuhusu matumizi ya vyandarua, ingekuwa ni vyema kama wataalamu wa afya watazunguka mbalimbali kote nchini kujionea hali halisi na kutoa elimu.

Shirika la Umoja wa Mataifa Linalowahudumia Watoto (UNICEF), lilishaweka wazi kuwa vyandarua maalum vilivyotengenezwa na kunyunyiziwa dawa ya kuua mbu, vinaokoa maisha ya wanavijiji wengi hapa nchini.

UNICEF iliwahi kukaririwa na Shirika la Habari la Ujerumani (DW) katika moja ya maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani, ikisema malaria imekuwa ukiua watoto chini ya umri wa miaka mitano, wazee, kinamama wajawazito na kwamba vifo hivyo, vimeanza kupungua baada ya matumizi ya vyandarua.

Hivyo basi, ni muhimu kwa jamii ikakubali kuwa na elimu sahihi kuhusu matumizi ya vyandarua, ili kuondoa imani potofu ambayo inawezekana, kwa namna moja au nyingine, inayochangia kuendelea kuwapo kwa ugonjwa huo nchini.

# DPP aondoa kesi ya mashtaka 209 ya watumishi wa Maliasili

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI wa Mashtaka nchini (DPP) ameiondoa kesi ya uhujumu uchumi iliyosomwa juzi dhidi ya watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka 209 yakiwamo ya kujipatia zaidi ya Sh. bilioni 4.3.

Shauri hilo liliondolewa jana baada ya upande wa Jamhuri kuomba mahakama iliondoe mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Eliud Kijalu na Daudi Mpangile waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka 209, yakiwamo kuongoza genge la uhalifu, kughushi na kujipatia fedha zaidi ya Sh. bilioni 4.3 kwa njia ya udanganyifu.

Juzi washtakiwa hao walifikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka 30. Mashtaka mengine yaliyobaki yalitarajiwa kusomwa jana lakini hayakusomwa.

Akitoa taarifa mahakamani huko, Wakili wa Serikali Mkuu, Saraji Iboru, alidai walipokea taarifa kutoka upande wa upelelezi kwamba kuna washtakiwa wengine watano wanaopaswa kujumuishwa katika kesi hiyo, hivyo wameona si busara kuendelea na mashtaka hayo mpaka hao wengine watakapounganishwa.

"Mheshimiwa Hakimu, tumepata taarifa kuna washtakiwa wengine watatu wanatakiwa kuunganishwa na wengine wawili hawajaripoti.

"Kwa kuzingatia wingi wa mashtaka na kuokoa muda wa mahakama, tunaomba kwa mamlaka ya kisheria aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu 91(2) cha Sheria ya Makosa ya Jinai, kuondoa shauri hili. Tutakapokuwa tayari tutalirejesha," alidai.

Upande wa utetezi haukuwa na pingamizi , mahakama ilikubali maombi hayo na kuondoa shauri.

"Kama alivyosema Wakili wa Serikali, chini ya kifungu 91(1), DPP anayo mamlaka ya kuondoa shauri mahakamani. Mahakama inaliondoa shauri na washtakiwa wanaachiwa, lakini hii haimaanishi kwamba ninawaachia huru, mnaweza kuitwa wakati wowote," alisema hakimu huyo.

**Kwa kuzingatia wingi wa mashtaka na kuokoa muda wa mahakama, tunaomba kwa mamlaka ya kisheria aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu 91(2) cha Sheria ya Makosa ya Jinai, kuondoa shauri hili. Tutakapokuwa tayari tutalirejesha.**




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili (kushoto), akikabidhi ufunguo na namba za usajili wa gari aina ya Toyota Crown kwa Jared Awando Ojweke aliyeibuka mshindi wa kampeni ya Benki ni Simbanking, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgogoro CWT watinga bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kufanya kazi kwa karibu na vyama vya wafanyakazi kwa kusuluhisha migogoro iliyoko, ikiwaomba walimu kuendelea kukiamini chama chao (CWT).

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge, Ummy Nderiananga, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mbunge huyo alitaka kujua kauli ya serikali kuhusu ulazima wa kujiunga na vyama vya wafanyakazi na itoe tamko la kuruhusu mwalimu kujiunga na chama chochote anachoridhika nacho.

"Katika hivi vyama ulazima upo maana mfanyakazi anapoingia tu katika ajira anakatwa fedha za kujiunga na chama bila ridhaa yake, kama sio lazima unaweza kutoa tamko leo ili mwalimu yeyote aingie chama chochote anachotaka yeye?" alihoji.

**Ada za wanachama hutumika kutekeleza majukumu ya vyama yaliyowekwa kikatiba na kisheria yanayotokana na kuwapo vyama mahala pa kazi.**

Akijibu swali hilo, Ummy alisema zipo katiba zinazoongoza vyama vya wafanyakazi na serikali inafahamu kuna baadhi ya vyama vina migogoro. Itaendelea kufanya kazi kwa karibu na vyama hivyo kwa kuboresha penye upungufu, pia kusuluhisha migogoro inayoendelea katika vyama husika.

"Niwatoe hofu walimu waendelee kukiamini chama chao cha walimu na sisi serikali tupo pamoja nao," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mwandabila, alitaka kujua faida ambayo wafanyakazi wanapata kupitia uwekezaji wa fedha katika vyama hivyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ummy alisema faida ambayo wafanyakazi wanapata kupitia uwekezaji wa fedha wanazokatwa na vyama vya wafanyakazi ni kusuluhisha migogoro ya kikazi kwa niaba ya mwanachama wake, kutoa huduma kwa wanachama, kutoa elimu kuhusu sera na sheria za kazi kwa ajili ya maslahi mapana ya wafanyakazi.

Pia alisema ada za wanachama hutumika kutekeleza majukumu ya vyama yaliyowekwa kikatiba na kisheria yanayotokana na kuwapo vyama mahala pa kazi.

"Vipo baadhi ya vyama vya wafanyakazi ambavyo hutumia ada za uanachama kujenga majengo kwa ajili ya matumizi ya ofisi za vyama, kuwapangisha watu mbalimbali na kutoa huduma kwa wanachama wao na fedha inayopatikana hutumika kusaidia bejeti za vyama," alisema.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# 'Mafunzo ya JKT siyo mateso yanaandaa vijana kulinda taifa'

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Tawi wa Utawala, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali Hassan Mabena, amesema mwaka 1994 serikali ilipositisha mafunzo ya JKT kwa vijana wanaohitimu kidato cha sita, kuliibuka mmomonyoko wa maadili kwa taifa ikiwamo migomo vyuo vikuu.

Pia amewakumbusha wazazi na walezi kwamba mafunzo hayo ni silabi inayozingatia viwango na afya na utimamu wala siyo mateso, yanalenga kuwaandaa vijana wao kuwa wastahimilivu na wakakamavu kwa ajili ya kutumikia na kulinda taifa.

Aliyasema hayo juzi wakati jeshi hilo likitangaza kusitisha kupokea tena vijana walioitwa kujiunga na mafunzo hayo kwa mwaka 2023.

"Vijana ambao walishindwa kuripoti kwa muda waliopangiwa hawatapokewa kambini hivyo, wasiende kuripoti. Jeshi lilitoa wito kwa vijana wote waliohitimu elimu ya kidato cha sita kwa mwaka 2023 kutoka shule zote Tanzania Bara, kufika katika kambi walizopangwa.

"Sanjari na wito huo, JKT iliwapangia kambi watakayokwenda kupatiwa mafunzo na tarehe ya kuripoti kambini ilikuwa ni Juni Mosi hadi Juni 11 mwaka huu," alisema.

Brigedia Jenerali Mabena alisema vijana ambao walishindwa kuripoti kwa muda waliopangiwa hawatopokewa kambini, hivyo wasiende kuripoti.

Alisema kukosa mafunzo kwa vijana hao ambao hawajahudhuria kambini ni kukosa uzalendo, ndio maana wanasisitiza muda ni kitu cha muhimu kuzingatiwa.

"Wazazi na walezi wasisubiri kinachoonekana hapa wanasubiri kuripoti mwishoni na wengine wanakuwa hawana sababu za msingi, wanachelewa tu, hivyo inaathiri pia utoaji wa mafunzo. Mafunzo yanapoandaliwa wale watakaoitwa waripoti mara moja," alisisitiza.

Alisema mafunzo hayo yalipositishwa mwaka 1994, kulitokea madhara makubwa ya mmomonyoko wa maadili kwa taifa. Hivyo serikali imeyarejesha kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita.

"Ikumbukwe kuwa kati ya mwaka 1994 kuelekea mwaka 2013 migomo vyuo vikuu ilikuwa ya hali ya juu. Utandawazi pia ni tatizo, vijana wamekuwa wakipata taarifa za mataifa mbalimbali ambapo mengine utamaduni wao hauendani na wa kitanzania. Mmomonyoko wa maadili uliongezeka, nidhamu kazini na uzalendo ulipungua," alisema.

Alisisitiza lengo la kuweka ukomo wa kuripoti kambini ni kuendana na silabi ya mafunzo ya vijana wa JKT kwa mujibu wa sheria ambayo ni miezi mitatu tu.

Alisema kuwa baada ya vijana kuripoti kambini, taratibu za kuwafanyia vipimo vya utimamu wa mwili hufanyika kabla ya kuanza mafunzo rasmi.




Meneja Unadi wa Kampuni ya ALAF Tanzania, Salwa Omari (wa nne kulia), akikabidhi msaada wa vitabu 200 vyenye machapisho ya miswada ya washindi wa Tuzo ya Kiswahili ya Safal-Cornell ya Fasihi ya Afrika 2022 kwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Dar es Salaam (Utafiti), Prof. Nelson Boniface, kwa ajili ya maktaba ya chuo hicho juzi. Wengine (kutoka kushoto) ni Mhadhiri Mwandamizi wa UDSM, Dk. Mussa Hans, mmoja wa waandishi wa vitabu Hafidh Kido, mwakilishi wa maktaba ya UDSM Magreth Bwathondi, Mkurugenzi TATAKI, Prof. Shani Omari Mchepange na Ofisa Uhusiano wa ALAF Theresia Mmasy. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ajira mpya 45,000 kutolewa kutatua uhaba wa watumishi

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi na Utawala bora, Ridhiwani Kikwete amesema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 serikali ina mpango wa kuajiri watumishi wa umma 45,000 ili kukabiliana na upungufu uliopo.

Ridhiwani alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kyerwa (CCM), Innocent Bilakwate.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kuongeza watumishi katika sekta ya elimu na afya ili kukabiliana na upungufu katika Wilaya ya Kyela.

Pia alitaka tamko la serikali kuhusu watumishi 18 katika wilaya hiyo waliostaafu mwaka 2018, wakiwamo watendaji wa kata, ambao mpaka sasa hawajalipwa mafao yao.

"Serikali ipo tayari kuwapandisha vyeo kwa mserereko hadi kufikia daraja ambalo wangestahili watumishi ambao wamesubiri zaidi ya miaka minane wilayani humo?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeendelea kupandisha madaraja watumishi wake na kuajiri watumishi wanaohitajika na katika bajeti ya mwaka 2022/23 ilitoa vibali vya ajira 30,000 kwa ajili ya kuongeza watumishi.

"Ninataka niwahakikishie wabunge pamoja na Bunge lako kwamba serikali itaendelea kukabiliana na upungufu wa watumishi katika sekta zote zilizopo nchini," alisema.

Pia aliwataka watumishi hao ambao hawajalipwa mafao yao kupeleka barua zao kwa Katibu Mkuu Utumishi ili wapate stahiki zao.

Kuhusu upandishwaji vyeo kwa mserereko, alisema ni utaratibu unaotumika kuwapandisha vyeo watumishi ambao imethibitika walicheleweshwa kupandishwa vyeo kwa wakati kwa kuzingatia miongozo ya upandishaji vyeo iliyopo.

Alitaja miongozo hiyo kuwa ni kuwapo nafasi iliyoidhinishwa katika ikama na kuwapo fedha za kugharamia upandishwaji vyeo katika bajeti, sifa za kielimu na kitaaluma na utendaji kazi mzuri.

# RC aagiza kujibiwa hoja za CAG

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Maryam Muhaji, kuhakikisha hoja zote zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinajibiwa ili zifungwe.

Kiongozi huyo aliagiza hayo alipotoa salamu za serikali katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe kilichofanyika kwa lengo la hoja za CAG.

"Hongereni kwa kupata hati safi lakini kikubwa hoja zote zijibiwe na tuzifunge ili mkurugenzi tunapokwenda katika vikao mwakani kwenye Bunge la Bajeti, tusiwe na doa, aliagiza.

Awali Mwekahazina wa halmashauri hiyo, Nickson Itogolo, akiwasilisha hoja ambazo hazijafungwa, alisema halmashauri ilikuwa na hoja 32 za miaka ya nyuma.

"Hadi sasa hoja 27 zimefanyiwa kazi na kufungwa na kubakiwa na hoja tano ambazo zipo katika hatua ya utekelezaji," alisema Itogolo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Agnetha Mpangile, alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo kwa kila kata.

"Kwa muda huu mfupi kabla ya kufunga mwaka, tuhakikishe kila kijiji, kila kata inasimamia kwa weledi mapato na matumizi," alisisitiza Mpangile.



## Wananchi waridhishwa huduma kambi madaktari bingwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANANCHI wa Mkoa wa Manyara, wamesema wameridhika na huduma inayotolewa na jopo la madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, ikiwamo za kibingwa kwa wagonjwa kupitia kambi maalum ya matibabu na madaktari bingwa wa mama Samia Kanda ya Kaskazini.

Baadhi ya wananchi hao walisema hayo jana, wakati wakizungumza na Nipashe ilipokuwa ikifutilia namna huduma hiyo inavyotolewa.

Mkazi wa Babati, Chiku Shaban, alisema huduma ilivyotolewa na madaktari bingwa inakidhi vigezo na wanandelee kuwahudumia wananchi kwa kuwafuata mikoani.

"Serikali iwe inatoa huduma hii mara kwa mara kwa kuwa wananchi wengine hatuna uwezo wa kwenda Hospitali za KCMC, Muhimbili, Benjamin Mkapa au Bugando kwa kuwa gharama inakuwa kubwa," alisema Shaban.

Mkazi wa Kijiji cha Gallapo, Maulid Salim, alisema alipokewa vizuri na wahudumu wa hospitali hiyo na kuwaona madaktari bingwa.

"Nimeridhika na huduma hii inavyotolewa na ikiwamo lugha nzuri inayotolewa na wahudumu na madaktari hao ni nzuri mno, hivyo naomba waendelee hivi hivi kutuhudumia," alisema Salim.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, bingwa wa magonjwa ya wanawake alisema, mara nyingi kinamama wakifika hospitalini wanakuwa na shida ya kupata watoto kwa kuwa inasababishwa na uambukizi wa bakteria kwenye via vya uzazi.

"Mtu anayechelewa kupata ujauzito aje hospitali kufanya uchunguzi na kuhusu uambukizi ni vizuri kutumia kinga kupata bakteria," alisema Dk. Magali.

Aidha, alisema kutokana na wanawake kuendelea kushambuliwa na ugonjwa wa UTI, aliwashauri waendelee kufanya usafi sehemu ya haja ndogo na kubwa kwa kuwa vimekaribiana na kuwa rahisi kupata maambukizi.

Alisema kwenye kambi hiyo, wanatoa huduma kuanzia saa 11:00 asubuhi na kuna wagonjwa wanahitaji upasuaji na wengine kutaka kuchunguzwa magonjwa ya ndani.

Katibu wa Afya wa hospitali hiyo, Sakina Kiponza, alisema madaktari bingwa waliofika kutoa huduma wako 33 na watatoa huduma kuanzia Juni 12 mpaka Juni 16, mwaka huu.

# Atupwa jela miaka 20 kukutwa akitafuta mteja meno ya tembo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 20 kwenda jela mkazi wa Kijiji cha Magugu, Gurtu Sirro (33), kwa kosa la kukutwa na vipande vitatu vya meno ya tembo akiwa anatafuta mteja wa kumuuzia.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na hakimu mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Victor Kimario.

Kimario, akisoma hukumu hiyo ya uhujumu uchumi ya mwaka 2023, alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Januari 17 katika Kijiji cha Matufa, wilayani Babati.

Alisema mshtakiwa alikutwa amebeba meno matatu ya tembo yenye uzito wa kilogramu 35 ambayo thamani yake ni Sh. milioni 45.114.

**Nakutia hatiani pasipo kuacha shaka baada ya kujiridhisha kusikiliza upande wa mashtaka ambao umethibitisha kuwa ulikutwa na meno matatu ya tembo.**

Aidha, alisema shahidi namba tatu, nne na tano walimkuta mshtakiwa akiwa amebeba mzigo huo na shahidi wa tatu alijifanya mteja na kumnasa mshtakiwa.

"Nakutia hatiani pasipo kuacha shaka baada ya kujiridhisha kusikiliza upande wa mashtaka ambao umethibitisha kuwa ulikutwa na meno matatu ya tembo," alisema Kimario.

Kimario alisema mshtakiwa alikiuka Sheria ya Wanyama pori kifungu cha 86(1)(2)(b) sura ya 283 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022, ikisomeka na aya ya 14 na kifungu cha 57(1) na kifungu cha 60 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi sura ya 200 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Awali, Wakili wa Serikali, Rusticus Mahundi, akisaidiana na wakili mwenzake wa serikali, Abood Komanya, alidai kuwa mshtakiwa hana kumbukumbu za makosa ya nyuma kwa kuwa tembo ni wachache na ni kivutio cha utalii na watalii wanaliingizia taifa fedha nyingi za kigeni na kutaka mahakama itoe adhabu stahiki ili iwe fundisho.

Mahundi, aliiomba mahakama irudishe nyara hizo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Wanyamapori ili itumiwe kwa usahihi.

Alipopewa nafasi ya kujitetea, Gurtu Sirro, alisema anategemewa na familia na ana watoto wanne ambao mama yao alishafanyiwa upasuaji mara nne hivyo hawezi kufanya kazi yoyote anamtegemea yeye, aliomba mahakama imwachie huru.




Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Kheri James (aliyesimama), akizungumza na vijana 139 washiriki wa mafunzo ya utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, yaliyofanyika bonde la Yaeda Chini juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tatizo la uzazi lawaibua wawekezaji sekta afya

**Na Oscar Assenga,** TANGA

TATIZO LA uzazi na ugumba limewaibua wawezekezaji katika sekta ya afya mkoani Tanga, kwa kuanza kufanya uwekezaji ambao utasaidia kutokomeza adha waliokuwa wakiipata wananchi kusafiri nje ya nchi kufuata huduma hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Hospitali ya Safi Medic's iliyoko jijini Tanga, Joseph Mberesero, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya ufunguzi wa jengo la kutolea huduma za nje (OPD), ambalo lilifunguliwa na mbio za Mwenge.

Alisema uzazi na ugumba ni tatizo kubwa na wananchi wanahangaika kwenda nje na ndani ya nchi kutafuta huduma hizo, wametambua na wameamua kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi.

Alisema wataanza hospitali hiyo itakayokuwa na uwezo wa kuwahudumia kinamama wenye matatizo tofauti ikiwamo upandikizaji wa mtoto kwenye muda husika na wataendelea kuwekeza kwenye eneo hilo, ili kuhakikisha wananchi wa mkoani humo wanapata huduma bora za afya.

"Kwa kweli tumeamua kujikita zaidi katika huduma za kinamama na watoto kwa kutoa kliniki za wajawazito, ugumba na tunafanya upasuaji wa dharura kwa kinamama wenye ujauzito na wasiokuwa nao," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa wana wagonjwa watakao kuwa wakiwahudumia kupitia jengo la OPD litakalokuwa na kliniki ya kinamama na wagonjwa wengine ikiwamo huduma ya kusafisha figo, huduma ya madaktari wa pua, koo, masikio na ultra sound.

"Magonjwa nyemelezi ni tatizo kubwa nchini kwa kuwa inaonekena watu wengi wanapata matatizo ya kufeli kwa figo na wanahitaji kusafisha figo na huduma hiyo, ilikuwa inapatikana eneo moja, tumeona tupanue wigo kuhakikisha huduma hiyo inapatikana hapa," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa wako kwenye mchakato wa kusajili ili iweze kuwa hospitali ya wilaya kwa kuwa huduma zao watoa huduma za nje na kulaza wagonjwa ikiwamo kufanya upasuaji wa magonjwa yote kwa kuwatumia madaktari bingwa wa magonjwa mbalimbali ya wanawake, mifupa, ngozi, magonjwa ya ndani, uzazi na ugumba.





# Bil. 7/- zawekezwa kilimo umwagiliaji Nzega

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI imetoa Shilingi bilioni saba kwa ajili uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mbegu Kilimo, wilayani Nzega, mkoani Tabora kuongeza uzalishaji kwa kipindi chote cha mwaka bila kutegemea misimu ya mvua ambayo inabadilika kulingana na mabadiliko ya tabianchi.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo Nchini (ASA), Dk. Sophia Kashenge, akizungumza wakati wa ukaguzi wa mradi huo wenye ukubwa wa ekari 1,000, alisema fedha hizo lengo lake ni kuongeza uzalishaji wa mbegu na kuacha kutegemea mvua za masika.

Alisema, uzalishaji utaongezeka kutoka tani 200 zilizokuwa zinazalishwa kwenye hekta 200 hadi tani 1000 kwenye hekta 200 na huo ni wastani wa chini wa uzalishaji.

**Wananchi wa mkoa huu walio wengi ni wakulima lakini bado wanakabiliwa na ukosefu wa masoko hivyo tunaomba suala hili ulivalie njuga.**

Dk. Sophia alisema, shamba hilo litakapokamilika ufungaji wa miundombinu hiyo katika hekta zote 400 uzalishaji utaongezeka maradufu na upatikanaji wa mbegu kwa ukanda wa Ziwa na Magharibi ya nchi.

Aidha, alionesha kuridhishwa na kazi inayoendelea ya uwekaji wa miundombinu hiyo inayosimikwa chini ya usimamizi wa Kampuni ya Pro Agro Global Ltd.kufikia asilimia 57.

Mitambo ya Pivot minne kati ya saba imefungwa katika awamu ya kwanza shambani huku mingine mitatu ikiendelea kufungwa.

Alisema ifikapo mwezi Julai, kazi ya umwagiliaji itakuwa imeanza katika eneo la hekta 200 za awali huku zingine 200 zikiendelea kufungwa mitambo mingine saba ya awamu ya pili katika eneo lote la hekta 400.

Alisema kazi hiyo vilevile inaendelea katika mashamba ya Msimba Kilosa, mkoani Morogoro na Arusha Ngaramtoni, kazi zinaendelea kila shamba linawekewa umwagiliaji wa hekta 200 na kazi zimefikia asilimia 50.

Baadhi ya wakulima waliiomba serikali kuendelea kutoa taarifa ya mabadiliko ya hali ya hewa ili kuwapa mwanya wa kufanya shughuli za kilimo kwa wakati mwafaka wakati wakiendelea kusubiri miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa ili kuboresha kilimo.



Vibarua wakishusha mabomba ya kusambaza maji, kwa ajili ya vijiji vya kata za Mugango na Tegeruka mwishoni mwa wiki, vinavyopitiwa na mradi wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Mugango-Kiabakari hadi Butiama mkoani Mara, wenye thamani ya Sh. bilioni 70.5, uliozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwanzoni mwa mwaka jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ualbino waomba kutobaguliwa ajira

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha Watu wenye ualbino wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, kimelalamikia kitendo kinachofanywa na baadhi ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayowabagua watu wenye ualbino kutoshiriki shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo ajira licha ya kuwa na uwezo wa kufanyakazi kama makundi mengine.

Mwenyekiti wa chama hicho, Nisher Fabiani, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu wanavyokabiliana na changamoto ya unyanyapaa ndani ya jamii hususani kutoshirikishwa katika shughuli mbalimbali kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya albino dunia yenye kaulimbiu "Ujumuishi ni Nguvu".

Alisema, licha ya kusoma na kuwa na viwango vikubwa vya elimu, wanabaguliwa katika upande wa ajira kwa kigezo kuwa hawawezi kufanyakazi muda mrefu hususani wakiwa juani hali inayowafanya kujiajiri na kuondokana na dhana ya kutegemea ajira kutoka serikalini au mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

"Suala la ajira kwa wetu wenye ualbino bado halijakaa sawa, tunabaguliwa hata na baadhi ya mashirika ambayo yanafanya shughuli zao ndani ya jamii, kwa kigezo hatuwezi kufanyakazi muda mrefu na tukiwa juani, ni wajibu wa serikali kuingilia katika na kutatua tatizo hili," alisema Fabiani.

Hata hivyo, aliomba kupewa ajira kulingana na viwango vyao vya elimu kwa kuzingatia vigezo vya ajira vinavyohitajika kwa mujibu wa sheria ili waweze kukidhi gharama za kununua mafuta ambayo yanawasaidia kujikinga mionzi ya jua ili ngozi zisiharibike na kupata kansa.

Alisema, kwa sasa wanatarajia kuanzisha mradi wa ufugaji nyuki, baada ya kuvuna na kuuza asili, fedha zitazopatikana watanunua mafuta kinga kwa wingi na kupeana wao kwa wao ili kujikinga wasiendelee kupata kansa ya ngozi kwa kupata vitu ambavyo sio sahihi katika ngozi zao.

Naye Sada Mwasulama, mkazi wa kijiji cha Iyenye Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, alisema wanaoishi pembezoni mwa mji wanasumbuka kupata mafuta kinga kukabiliana na saratani ya ngozi na badala yake wanalazimika kupata mafuta ambayo sio sahihi na kuwababua na kuharibika.

Alisema, hata kwenye kazi ndogo ndogo, hawapewi kipaumbele kwa madai wao hawawezi kufanyakazi kwa muda mrefu hasa juani na kuiomba serikali kuingilia kati kutatua tatizo hilo kwa kuwa fedha wanazozipata wanazielekeza katika ununuzi wa mafuta.

# Mradi ufugaji nyuki Msalala wainua kipato

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

UTEKELEZAJI wa Mradi wa ufugaji nyuki kwa wananchi wa Kijiji cha Buyange, Kata ya Bugarama, Halmashauri ya Msalala, umesaidia kuinua hali yao ya kiuchumi kwa asilimia kubwa na kuwasaidia kujikwamua katika maisha yao.

Katibu wa kikundi cha ufugaji nyuki cha Twikondele, Daniel Samson, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kikundi hicho kinacho fadhiliwa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, unavyo wasaidia wananchi wanaozunguka mgodi huo kuwainua kiuchumi.

Alisema kikundi chao kilianzishwa mwaka 2015 na kupewa mizinga 17 ya nyuki, ambayo wanavuna asali na kuiuza kwenye masoko ya ndani na kujipatia kipato kinachowasaidia kuinuka kiuchumi na kuendesha maisha yao.

"Kikundi chetu cha ufugaji nyuki tupo watu 13 na fedha ambazo tunazouza asali tunajikopesha wenyewe kwa wenyewe na kuendelea kuizalisha kwa kuweka akiba benki na nyingine kugawana na kuzitumia kwa kuendesha maisha yetu na kuhudumia familia," alisema Samson.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Belta Ndeki, alitaja mafaniko ya kimaendeleo wanayoyapata kupitia ufugaji nyuki, kuwa baadhi ya wanakikundi wamejenga nyumba imara na kuondoka kwenye nyasi, kununua mashamba pamoja na kusomesha watoto kwa kuwatimizia mahitaji yao ya shule.

Kaimu Meneja Mahusiano ya Jamii Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Zuwena Senkondo, alisema mgodi huo umeendelea kuwa karibu na jamii kwa kuwajengea uwezo na kukuza uchumi wao na katika uwezeshaji wa jamii kupitia ufugaji nyuki, wametoa mizinga 200 kwa vikundi vitano.

Alisema, kupitia ufugaji nyuki, wanawapeleka wanakikundi katika maonesho mbalimbali ya biashara ili wakajifunze kwa wenzao pamoja kupata mtandao na kupanua wigo wa biashara zao.

**Kikundi chetu cha ufugaji nyuki tupo watu 13 na fedha ambazo tunazouza asali tunajikopesha wenyewe kwa wenyewe na kuendelea kuizalisha kwa kuweka akiba benki na nyingine kugawana na kuzitumia kwa kuendesha maisha yetu na kuhudumia familia.**

ama
ALHAMISI JUNI 15, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



## Wadau na serikali wakaa pamoja kutathmini hali ya Ukimwi kitaifa

Ukurasa 12



## HARAKATI ZA MAZINGIRA NCHINI... Yalivyo mapambano kudhibiti uchafu uliosheni kwenye fukwe zilizoko nchini

Ukurasa 13

# Mpango MAMM uliobuniwa awamu ya nne, Rais aunoa kuboreshea afya ya leo

• Mapya zahanati, hadi Muhimbili na pacha zake

**Na Mwandishi Wetu**



Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi, mjini Mpanda katika hatua za ujenzi hadi kufika, Desemba mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

SEKTA ya afya daima imekuwa marejeo na eneo muhimu katika maendeleo ya nchi, pia kipaumbele katika miaka yote 62 ya uhuru wa nchi.

Katika zama za awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi, mwasisi wa taifa, Rais Julius Nyerere, kama ilivyo maendeleo ya maeneo mengi, akaelekeza zaidi mikakati ya maendeleo ya sekta hiyo kwenye afya ya msingi.

Hicho ndicho kikatawala, hasa katika mipango mikuu miwili ya kwanza ya maendeleo ya miaka mitano kila moja, kuanzia mwaka 1964.

Hapo ndio zao lake, mathalan jijini Dar es Salaam kukashuhudiwa ujenzi wa zahanati pacha za Mnazi Mmoja, Amana, Temeke na Mwananyamala, ambazo zote sasa zina hadhi za hospitali. Pia, mjini Tanga kukawapo pacha wao, Zahanati ya Chumbageni.

Vilevile katika awamu hiyo ya kwanza ya uongozi wa nchi, maboresho ya kuasisiwa nyenzo za afya ya msingi, yakaendana na elimu ya msingi, yakaendana na elimu na kampeni maalum, pia ikiingizwa hata kwenye mitaala ya elimu ya msingi, kufafanuliwa redioni na bendi za dansi nazo hazikuwa nyuma kuelimisha kupitia muziki.

Kadri muda ulivyosonga, kukashuhudiwa mageuzi na maendeleo, pia mahitaji mapya ya wakati husika. Hata ilipofika, katika zama za uongozi wa nchi awamu ya nne, kukafanyika maboresho ya ubunifu wa awali, kwa kuanzishwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ulioidhinishwa mwaka 2007 na kuanza kutumika mwaka mmoja baadaye.

MMAM nayo ikaandaa muundo unaotumika sasa, kwamba zahanati ikatakiwa katika kila kijiji na kitongoji, huku ngazi ya kata kunakuwapo kituo cha afya.

Vilevile, kukitajwa wilaya inapaswa kuwa na hospitali na ngazi ya mkoa kunakuwapo hospitali ya rufani, juu yake katika kanda zinakuwapo hospitali za rufani na mamlaka ya juu kitaifa ni Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Matokeo ya maboresho hayo, ikazipa hadhi kuwa hospitali za rufani za mkoa, kama zile za wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni, ambazo mzizi wake ulianzia kwenye zahanati.

**KILICHOKO SASA**

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiendelea na mikakati yake katika awamu ya sita, anachambua MMAM katika baadhi ya maeneo, akitaka huduma ya afya inayojitosheleza na yenye tija.

Muda mfupi baada ya kuingia madarakani, Rais wa awamu ya sita akazamisha juhudi katika sura kuu tatu, ambazo nazo zikiwa za mwendelezaji wa yale ya mtangulizi wake, tangu yeye akiwa Makamu wa Rais, mwaka 2015.

Hapo Rais Dk. Samia akajikita katika msingi, kutimiza idadi ya zahanati na vituo vya afya penye mapengo, mahitaji ya msingi kwa dawa na vifaa muhimu vya tiba.

Katika ngazi ya juu, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na wabia wake, Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa Fahamu Muhimbili (MOI), vilevile Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, akizipa uwezo kimataifa.

Hapo inajumuisha mafunzo ya ziada, nao wakirejesha ujuzi huo ngazi ya chini na zinapewa ushirikano kimataifa na kuingia kwenye utalii tiba, unaoshuhudiwa zaidi katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.

Kunatajwa kuna wagonjwa kutoka nchi jirani wakifika nchini kupata tiba, pia madakatari wa nchini wanavuka mipaka kwenda nchi jirani kama vile Malawi walikoweka kambi ya matibabu ya moyo.

Lingine la kuendeleza MMAM, ni maboresho makubwa kutimiza mapengo ya mahali kulikosekana hospitali, mathalan ujenzi unaokamilika sasa wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi, mjini Mpanda.

Vilevile katika sura ya zahanati na vituo vya afya, kuna kazi ama inaendelea au imekamilika katika mwaka ulioko wa fedha ya ujenzi na ukarabati katika mikoa yote 26 nchini, kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Rais (Tamisemi).

Pia, ndani ya kuboresha dira ya MMAM, ni pale namna ujuzi unaopatikana kupitia ngazi za maboresho ya taasisi za tiba ngazi za kitaifa katika uzio wa Muhimbili, Rais Dk. Samia ameweka mikakati kupitia Wizara ya Afya, ujuzi huo na stadi za ziada madaktari wanaenda kupiga kambi mbalimbali, hasa katika hospitali za mikoa, kusambaza stadi kwa madaktari na wataalamu walioko huko.

**UJUMBE KWA UMMA**

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika hilo anawataka wafanyaka-

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Wadau na serikali wakaa pamoja kutathmini hali ya Ukimwi kitaifa

## • Penye maeneo ya starehe bado tatizo



Waziri wa Afya Ummy Mwalimu (katikati),akiwa na ugeni kutoka Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Ukimwi (USPEPFAR) Global Fund na UNAIDS, wakikitembelea Kituo Cha Afya cha Makole, jijini Dodoma. **PICHA: YASMIN PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

MARADHI Ukimwi sasa yana wastani wa miongo minne nchini, yanajulikana kuwapata zaidi wenye rika zote na hauna tiba. Mtu anapopima afya yake na akagundulika ana ugonjwa huo, kuna utaratibu wa dawa za kufubaza wadudu hao.

Hivyo, jamii inashauri kupima afya kila mara na mtu anapogundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo, ni rahisi kujitunza, ili asiweze kuwaambukiza wengine.

Faida ya mtu akigundulika kuwa na Ukimwi, inakuwa nafasi mojawapo ya kumuwezesha kujitunza na kuwalinda wengine dhidi ya maambukizi hayo.

Serikali imekuwa na mbinu endelevu za kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo kupitia vituo vyake vya afya, zahanati na hospitali ambazo kuna maeneo yametengwa kwa ajili ya kuwahudumia wahitaji, wakiwamo watoaji elimu ya ushauri nasaha kwa jamii.

Hospitali binafsi, nazo kama zilivyo za umma nazo zinatoa ushauri nasaha kwa ugonjwa huo, sambamba na dawa zimekuwa zikitolewa bure kwa wanaobainika kuwa na maambukizi yake.

Juhudi hizo ni sehemu ya mikakati kuwawezesha waliopata maambukizi wapate dawa na elimu ya kuwakinga wasipate magonjwa nyemelezi, ikiwamo hatua za kujilinda dhidi ya maambukizi mapya.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amebainisha kwamba wastani ulioko katika kila watu 100, wako 86 wanajitambua kuwa wana maambukizi ya Ukimwi, huku kati ya hao wanaojitambua wako asilimia 97 wanatumia dawa.

Ni tamko la Waziri Ummy, katika Kituo cha Afya Makole, jijini Dar es Salaam, akiambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Angela Kairuki, akiwa na ugeni kutoka Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Ukimwi USPEPFAR, Global Fund na UNAIDS jijini Dodoma.

"Tunawashukuru wadau wetu hawa kwa msaada mkubwa waliotupatia, ambao umeisadia Tanzania kupatikana kwa mafanikio makubwa ambayo yameweza kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU)," anasema.

Anafafanua, wanaotumia dawa wamefanikiwa kufubaza virusi hivyo, kwa kujiepusha na maambukizi ya magonjwa mengine na wanaweza wasiwaambukize wengine.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, lengo la mkakati huo nchini, ni kutathmini utendaji na utekelezaji wa afya, pia mapambano dhidi ya magonjwa ya Ukimwi, kifua kikuu na malaria kuona namna ya kupuguza kasi ya maambukizi ya magonjwa hayo.

Anaongeza kuwa, tatizo hilo limewakumba zaidi wanaume, hivyo serikali itaendelea kuchukua mikakati mbalimbali ya kuwashawishi wanaume kupima afya zao dhidi ya Ukimwi, ili kuweza kutambua hali zao.

"Pia, kundi lingine linalopata maambukizi kwa wingi, ni wasichana balehe ,ambao wanafanya kazi kwenye baa, hoteli, makasino na kwenye vijiwe. Kwa hiyo, hao nao tutaweka mikakati mbalimbali ya kuwafikia," anatamka.

Waziri anataja eneo la tatu, kwamba wanakoenda kulifanyia kazi, ni maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, akitaja dunia inataka wastani isivuke asilimia tano, lakini nchini Tanzania ni asilimia 6.5 ya watoto wanaozaliwa na maambukizi.

Hapo waziri anatoa wito kwa Watanzania kwenda kupima kujua hali zao na watakaobainika kuwa na matatizo, wanajua hali zao na dawa zipo na zinatolewa bila malipo, pia kuna vipimo vya kujipima mwenyewe, akitaka

Watanzania wajitokeze kupima afya zao katika vita kutokomeza Ukimwi, katika dira kuelekea mwaka 2030.

# MPANGO MAMM ULIOBUNIWA AWAMU YA NNE, RAIS AUNOA KUBORESHEA AFYA YA LEO

**Inatoka Uk. 11**

zi waliopo hospitalini, kujitoa zaidi kuokoa maisha ya watu, ili kufikia azma ya kuwa na jamii yenye afya bora.

Ni tamko lake Rais baada ya kutembelea Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe, kukagua ujenzi wa miundombinu mpya yenye thamani Sh. Bilioni 27.

Katika ujumbe huo unaosonga mbali kwa ngazi mbalimbali za tiba na afya kitaifa, Rais Dk. Samia, anawaambia watendaji wa hospitalini Njombe, kwamba amesikia changamoto zao kikazi zikiwamo mahitaji ya vitendea kazi, akiwaasa kuchapa kazi na serikali inaendelea kushughulika changamoto zao.

"Matakwa yenu tunayafahamu ikiwamo mahitaji ya vitendea kazi, tutakwenda kujitahidi kuyatimiza ili muweze kufanya kazi vizuri," anatamka Dk. Samia.

Ni mtazamo anaosafiri nao kimataifa, hata mnamo Oktoba mwaka jana kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Ubunifu wa Afya Duniani (World Innovation Summit for Health) uliofanyika jijini Doha, nchini Qatar.

Dk. Samia anaweka angalizo la haja ya kuwa na afya imara, akizitaka nchi zinazoendelea kuwekeza kwenye ubunifu utakaoimarisha na kuinua sekta ya afya, ili kuzipa uwezo wa kupambana na maradhi ya mlipuko.

Katika hilo anataja haja ya kuhamasisha mipango bora ya afya duniani, akirejea Tanzania imepanga kuongeza ushirikiano kufikia utekelezaji wa mpango wa Umoja wa Mataifa wa Mwaka 2030, ndani ya Tanzania malengo yakiwa mwaka 2025.

Anasisitiza ukuaji miji na utandawazi, unaifanya dunia kuingia katika changamoto za kupanga sera rafiki za afya, ikiwamo udhibiti wa magonjwa hatari kama ilivyokuwa kwa Kovid - 19, ulioacha funzo kwa mataifa duniani, hatua za kuchukuliwa, kutosubiri majibu kwa mataifa yaliyoendelea.

Rais anasema Tanzania kama zilivyo nchini nyinginezo duniani, imekuwa ikitumia kasi ya mabadiliko ya teknolojia kimataifa, kufanya ubunifu kupata tija kwenye sekta ya afya.

Hapo anaeleza: "Baadhi ya uvumbuzi ambazo zimekuwa na tija nchini ni mfumo wa simu wenye kumuwezesha mjamzito kuita usafiri kwa dharura na kupelekwa hospitali 'M-Mama' pamoja na teknolojia inayotembea ya kulea watoto wanaozaliwa kabla ya wakati."

Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, ni teknolojia inayotoa majibu katika kupunguza vifo vya wajawazito na watoto, hatua ambayo serikali inaendelea nayo kuhakikisha inasambaa katika pande zote za Muungano.

Anahitimisha kwa kutaja changamoto inayorudisha nyuma juhudi za ubunifu kwenye sekta hiyo, ni ukosefu wa wafanyakazi wajuzi, uhaba wa miundombinu, pia kukosekana fedha za kufadhili ubunifu,

MAZINGIRA

## HARAKATI ZA MAZINGIRA NCHINI...

# Yalivyo mapambano kudhibiti uchafu uliosheheni kwenye fukwe za nchini



Hali iliyoko katika ufukwe Rainbow, Mbezi Beach, , Dar es Salaam, uliojaa taka za plastiki zilizotumiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU..**

**Na Jenifer Gilla**

TAREHE 5 ya mwezi Juni, Tanzania kuliadhimisha miaka 50 ya Siku ya Mazingira Duniani, pale Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), lilipotaja kaulimbiu kutafuta suluhisho la kutokomeza taka za plastiki, zinazoonekana kuwa kero.

Ni utaratibu unaofanyika kila mwaka tarehe kama hiyo, lakini mwaka huu UNEP inaeleza lengo kuu ni kuikumbusha jamii kuwa ina mchango mkubwa katika uchafuzi wa mazingira, kwa kutumia vifaa vya plastiki, pia kwa serikali na aina ya biashara ndivyo vitaamua kukuza au kutokomeza tatizo hili.

Tanzania ni moja ya nchi zinazokabiliana na changamoto ya uwapo wa wingi wa taka za plastiki zinazozagaa mitaani na pembezoni mwa bahari, licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na mamlaka za mazingira kutokomeza.

Kuna juhudi zinafanywa na wadau wa mazingira wanaoingia mitaani kuhamasisha jamii kuondoa taka za plastiki katika mazingira yao, ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali kutokomeza uzagaaji wake. Hata hivyo, visiwani Zanzibar, kuna mafanikio makubwa yamefikiwa, kukabili shida hiyo ya plastiki.

### KUTOKA TAASISI

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mikakati ya Maendeleo Endelevu (TSDI), Fredy Kwezi, ni mmoja wa wadau hao anayesema kila mwezi wanahamasisha jamii kusafisha fukwe za Bahari ili kuweka mazingira hayo safi.

Anasema ni mkakati waliouanzisha miaka mitatu iliyopita, baada ya kuona hali ya fukwe kuwa mbaya, akitoa mfano fukwe za 'Rainbow' iliyoko Mbezi Beach, Dar es Salaam, zilikuwa zimetapakaa taka za plastiki kiasi cha kupoteza mvuto kwa wanaopenda kutelembelea, hasa wageni.

Kwezi anasema, kila walipokuwa wakienda kusafisha fukwe hizo wanakusanya wastani wa viroba 30 vya taka za plastiki na kila wanaporudi wanakuta taka zikiwa zimeongezeka, jambo linaloonyesha watu wanaendelea kutupa kila siku.

"Ilibidi tuanze kazi ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutunza yale mazingira na kuchagua viongozi watakaosimamia usafi, angalau sasa hivi uchafuzi sio mkubwa na watu sasa wanaonekana kufurahia fukwe na biashara ndogo ndogo zinafanyika bila kuchafua mazingira," anafafanua.

Mwingine, Mkurugenzi wa Kampuni ya Libe Greed Innovation, Liberatha Kawamala, inayokusanya plastiki zilizotumika na kutengeneza mapambo ya nyumbani ikiwamo maua ya plastiki, bustani ya plastiki na 'flakes'.

Kupitia ubunifu huo, Liberatha anapatia pesa kwa kuuza bidhaa hizo sehemu mbalimbali nchini, hali inayochangia kumwongezea kipato, pia inapunguza taka za plastiki zinazozagaa mitaani.

Liberatha anasema, taasisi inatoa elimu kwa waokota taka namna nzuri ya kukusanya na kujipatia kipato, hali iliyoongeza idadi ya waokota taka za plastiki.

### KUTOKA NEMC

Kwa upande, mwigine kuna Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), ambalo linafanya kazi ya kuondoa mifuko ya plastiki isiyo na viwango, ilikuwa ikiishia kuzagaa mitaani na kuharibu taswira ya mazingira.

Hadi sasa NEMC, imekuwa ikitembelea viwanda vinavyozalisha vifungashio hivyo na kuhakikisha vinazalishwa vyenye ubora unaotakiwa pamoja hali iliyochangia kutokomeza taka za aina hiyo. Pia, chombo hicho kimekuwa kikitoa elimu kwa jamii, kuhusu madhara ya taka za plastiki kiafya na kimazingira ikiwamo kutoa sumu inayoweza kusababisha kansa kwa binadamu na pia kuchafua mazingira.

Ofisa Mazingira wa NEMC, Kulthum Shushu, anasema baraza hilo sasa lipo katika mchakato wa kuandaa teknolojia ya kuteketeza taka zinazoonekana kero, hasa pampasi zinazozagaa kila sehemu nchini.

"Udhibiti wa hizi taka ngumu upo katika ngazi ya halmashauri, lakini tunashirikiana nao kwa kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya kuzagaa taka hizo kwa afya na mazingira. Pia, tunahakikisha plastiki zinazozalishwa au kuingizwa nchini zina viwango vinavyohitajika," anasema.

### NINI KIFANYIKE?

Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, anasema ingawa Tanzania imepiga hatua kutokomeza taka hizo kwa kuboresha sera na sheria, nguvu inahitajika kuongezwa katika utekelezaji wa sera hizo.

"Kwanza Tanzania imepiga hatua kubwa, nchi nyingi zinasifu hatua iliyofikia ya kuondoa mifuko ya plastiki isiyokuwa na viwango. Hii yote imetokana na kubadilishwa kwa sera na kuzifanyia kazi matakwa yake" anasifu Prof. Yanda.

Anashauri mamlaka zinazosimamia sera na sheria kutumia njia na nguvu iliyotumika kumaliza tatizo la mifuko ya plastiki isiyo na viwango, sasa kushughulikia chupa za plastiki, vifungashio na taka kero kwa mazingira.

Msomi huyo anadems, wakati wanazuia kuzaga huko, watoe bidhaa mbadala zinaziweza kupatikana kwa bei nafuu, akitoa mfano wa mifuko ya karatasi ambayo kwa sasa ni mbadala mkuu wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

Mtaalamu huyo wa mazingira, anapendekeza kuwapo teknolojia ya kutengeneza mifuko, itkayotumika kwa muda mrefu, ili kupunguzwa utupaji mifuko holela .

Mkurugenzi wa Shirika la Utu na Mazingira, Sarah Pima, anasema kuna haja ya kupunguza matumizi ya vifungashio vya chakula na kurudi katika utaratibu wa zamani wa kutumia udongo, kwa kuwa taka hizo zinaongoza kutupwa ovyo.

"Zile wanazosema 'take away' zinaishia kutupwa ovyo, ukienda baharini unakuta pembezoni kumejaa sahani na vikombe vya 'take away' na 'pempasi'. Hili ni tatizo kubwa sana , nafikiri hata kwenye 'pempasi' turudi kwenye utaratibu wa nepi kwa sababu taka hii ni kero kubwa" anasema Sarah.

Ripoti mpya ya Shirika la Umoja wa Mataifa kla Mazingira (UNEP), inaeleza kuwa uchafuzi wa plastiki unaweza kupunguzwa kwa asilimia 80 kufikia mwaka 2024, iwapo nchi na mashirika zikiweka sera thabiti na mabadiliko ya masoko, kwa kutumia teknolojia iliyopo.

Inapendekeza mabadiliko matatu kwenye mfumo wa biashara ambayo ni 'isha, kutumia tena' ikiwa na maana kutengeneza bidhaa zinaweza kutumika kila mara, mfano wa chupa kubwa za lita 13, zinawekea maji ya kunywa ambazo zikiisha maji, mteja anarudisha dukani na kupewa nyingine yenye maji.

Njia ya pili anataja ni kuchakata. Ripoti hiyo inasema, hilo linawezekana, iwapo serikali itaondoa ruzuku kwa baadhi ya mahitaji ya utengenzaji, kutekeleza yaliyomo kwenye mwongozo wa kukuza uchakataji, na hatua nyinginezo kuongeza kiwango cha plastiki inayoweza kuchakatwa kutoka asilimia 21 hadi asilimia 50

Njia ya tatu inatajwa na UNEP, ni kubadilisha kwa uangalifu bidhaa za mifuko ya plastiki na vitu vya plastiki vya kupakia chakula, kwa bidhaa zilizotengenezwa kutoka kwa nyenzo mbadala kama vile makaratasi au vitu vinavyoweza kuoza, plastiki iliyochakatwa. Hiyo inaweza kupunguza asilimia 17 ya ziada ya uchafuzi wa plastiki.

AFYA

# RC Fatma Mwasa aaga Moro akiwa na salamu za vita dhidi ya ukatili

**Na Christina Haule, Morogoro**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa, amewataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuwa mabalozi na mfano katika maeneo yao, kwa kutunza maadili, inayojumuisha upendo utakaosaidia kutokomeza mmomonyoko wa maadili na ukatili mkoani hapa.

Fatma anayehamia mkoani Kagera, anataja maadili mema yanapaswa kuwapo, dhidi ya ukatili kwa watoto, wanawake na wazee kutapungua au kumalizika.

Anasema wazazi na walezi wanao wajibu kulea familia kwa kumjali mtoto, akipatiwa mahitaji ya msingi na kumlinda dhidi ya ukatili na kuzungumza hatari zinazokabili, kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na kanuni zake.

Anasema wazazi na walezi wanapaswa kudumisha mila na desturi za zamani, kuwa karibu na watoto kuwalinda na kuwapatia mahitaji, sambamba na kuwafundisha mambo muhimu ya kujilinda na kujiepusha na vitendo vya ukatili kijinsia, kama vile kuacha kumruhusu mtoto kwenda maeneo hatarishi kwa usalama wake ikiwamo kwenye kumbi za starehe, ngoma, baa na vigodoro.

"Ndugu wazazi wenzangu watoto ni wetu sote ukiona mtoto wa jirani yako, anatenda uovu mkataze, ukiona mtoto wa jirani anaenda eneo hatarishi mrudishe, mkataze, watoto ni wetu sote, mtoto wa mwenzio ni mwanao" anasema.

Anasema kumekuwapo sababu mbalimbali za mmomonyoko wa maadili, ikiwamo changamoto za kiuchumi zinazofanya wazazi wa kike kukosa muda mwingi wa kushinda na watoto, kuwatazama, kuwahoji na kuwafundisha

"Sasa hivi kutokana na changamoto za kiuchumi, hilo limebadilika sana, wazazi au walezi wanatumia muda mwingi kwenye shughuli za kujiongezea kipato na kutumia muda mwingi kujiongezea vipato na kusahau wajibu wa kusimamia malezi na makuzi ya watoto wao na hivyo kupoteza maadili mema kwa watoto," anasema.

Pia, anakemea tabia ya baadhi ya wazazi kuwapa simu za mkononi watoto kwa michezo mbalimbali, inawafungulia nyendo zinazochochea tabia ya kuiga desturi na mila za kigeni zinazokinzana na zilizopo nchini.

### MWELEKEO WA UKATILI

Mwassa anasema, mmomonyoko wa maadili umeendelea kuwepo kutokana na ukosefu wa utu, malezi mema, heshima, kukosa hofu ya Mungu, vilevile kuwapo mila na desturi kandamizi na kuvunjika kwa ndoa, vyote vikiwa na athari kwa mtoto.

Kuhusu maadili, anaanika masikitiko yake kuwa matukio mengi ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto yanayoripotiwa kupitia mamlaka za serikali za mitaa, yamekuwapo yakihusisha wazazi au ndugu wa karibu wanapoishi kwenye familia husika na kutoa picha kuwa mapambano dhidi



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, ambaye sasa kahamishiwa Kagera. **PICHA: MAKTABA.**

ya mmomonyoko wa maadili sio kazi rahisi.

Anashauri ni lazima, jamii zikumbuke mifumo bora ya kimalezi ya zamani kutoka kwa wazee inayosababisha kupatikana kizazi bora chenye heshima na maadili sahihi.

Kwa mujibu wa Mwasa, mwaka 2021 mkoa wa Morogoro katika madawati ya jinsia na watoto ya polisi, jumla ya matukio 347 yaliripotiwa na mwaka 2022 na kati ya mwezi Januari hadi Aprili 2023, yakawa 303.

Mwassa anasema, jumla ya vitendo vya ukatili 648 vimeripotiwa mwaka 2023 na waathirika wakubwa ni watoto na vijana, akifafanua umri wao ni kuanzia miaka 18 na chini yake yalikuwa matukio 342; kwa vijana wa miaka 19 hadi 35 kukawapo matukio 210 na; huku wenye umri wa miaka 36 hadi 70, yakawapo matukio 96.

Anasema serikali imechukua hatua na hadi sasa jumla ya kesi 620 zimeshafunguliwa na watuhumiwa 388 wamekamatwa na wapo katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi pamoja na kesi.

Mwassa anasema, kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Aprili mwaka 2023, jumla ya matukio 648 ya ukatili yaliyoripotiwa, matukio 295 yalikuwa ni shambulio; 135 ubakaji; 100 mimba kwa wanafunzi; 30 ulawiti; 29 kwa wanafunzi; na 26 ya kutelekeza familia.

Anayataja matukio mengine ni kutorosha wanafunzi 13, kujaribu kubaka manane, ukatili dhidi ya watoto yako saba, kutoa mimba matatu na mawili ni ya kutupa watoto.

"Ndugu zangu mimba ni 100! Hii ni idadi kubwa sana, watoto wadogo 100 wamejazwa mimba, hawa Watoto wakipata watoto wenzao hawana uwezo wa kuwalea. Hapo ndipo mmomonyoko wa maadili unapoanza, mama anatangatanga kutafuta maisha na mtoto anaachwa bila malezi, hakuna familia tena hapo," anasema.

"Nitoe rai, ndugu zangu, mimba 100 hazivumiliki sababu ni kama watu wazima wote tuliopo hapa na hatujatimia 100 na hizo zote ni mimba na hapa tupo watoto, walimu, wazazi na walezi, na hizi nyingi ni za shule ya msingi na inaashiria ubakaji ni mwingi, anasema.

Anasema, mkoa umeendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kuwezesha uimarishaji familia kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, wadau wa elimu na viongozi wa dini, kulinda maadili ya kitanzania kwa kuanzisha programu ya malezi na makuzi ya mtoto.

Mwasa anasema, serikali imeendelea kuhusisha na kuratibu kamati za ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi zote kuanzia mkoa, halmashauri, kata na vijiji.

Huku akivishukuru vyombo vya Habari kwa kushirikiana na serikali kutoa elimu ya jamii katika eneo hilo, dhidi ya ukatili katika jamii.

### MWALIMU ANENA

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mafiga, Angel Issa, anasema suala la mmomonyoko wa maadili kwa shule za sekondari sio kubwa sana, kwa wanafunzi tofauti na shule za msingi sababu wao wana utaratibu wa kukaa nao kila mwezi na kuwapa elimu mbalimbali za kujilinda.

Anawaasa wanafunzi waondokane na tamaa na vishawishi vya kutaka kula vitu na kuwa na vitu vizuri bali waridhike na maisha ya nyumbani kwao huku wakiamini kwamba wakisoma kwa bidii watapata wanavyovitaka.

Pia, mwanafunzi wa shule hiyo, Elia Richard anawaomba wazazi au walezi wanaoamini katika imani potofu na kufikia hatua ya kuwabaka na kuwalawiti watoto wao, kuacha mara moja, hao wakabadilika kuwa karibu, kuwatunza na kuwaelekeza watoto wao

Kwa mujibu wa Shirika la kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) karibu asilimia 60 ya matukio ya ukatili wa kijinsia yanatokea nyumbani na asilimia 40 yanatokea shuleni.

## SHAIRI



## BURIANI LEILA SHEIKH, KAACHA ALAMA ZAKE

*Mwanaharakati nguli, mpambanaji mfano,*
*Mguu sawa kamili, kwa matendo hata wino,*
*Haki alizijadili, tena kwa bidii mno,*
*Amefariki Leila, iwe chachu kwa wengine.*

*Amefariki Leila, iwe chachu kwa wengine,*
*Watu wote makabila, waanze jali wengine,*
*Hadi iwe bilabila kuwanyanyasa wengine,*
*Leila kitabu chake, chetu wengine kusoma.*

*Leila kitabu chake, chetu wengine kusoma,*
*Livyofanya mambo yake, kwa vitendo na kusema,*
*Akijenga hoja zake, haki iweae simama,*
*Wino wake ni wa chuma, hauwezi kufutika.*

*Wino wake ni wa chuma, hauwezi kufutika,* .
*Kama TAMWA waisema, mmoja alisimika,*
*Hadi TAMWA kusimama, huyo alichakarika,*
*Kaacha alama zake, kwa hizo atakumbwa.*

*Kaacha alama zake, kwa hizo atakumbukwa,*
*Zile harakati zake, atazidi kutamkwa,*
*Na sisi hata wenzake, atazidi kuandikwa,*
*Yake changamoto kwetu, kwamba tutaacha nini.*

*Yake changamoto kwetu, kwamba tutaacha nini,*
*Katika maisha yetu, tunapigania nini,*
*Nini wataona kwetu, karaha au amani,*
*Maisha yetu kitabu, kinasomwa kitasomwa.*

*Maisha yetu kitabu, kinasomwa kitasomwa,*
*Twaishi tunaratibu, bila ya mtu kutumwa,*
*Leila chake kitabu, kimebakia kusomwa,*
*Andika tutakusema, kwa ubaya hata wema.*

*Andika tutakusema, kwa ubaya hata wema,*
*Kwa jinsi unavyosema, au kugoma kusema,*
*Shamba unavyolilima, mavuno yakasimama,*
*Leila ameondoka, tunamshukuru Mungu.*

*Leila ameondoka, Mungu tunamshukuru,*
*Duniani kumuweka, kupigania uhuru,*
*Kazi imekamilika, yake yabakia nuru,*
*Pole nyingi twazitoa, kwa ndugu hata jamaa.*

*Pole nyingi twazitoa, kwa ndugu hata jamaa,*
*Majonzi hayajapoa, kifo kwetu ni balaa,*
*Mungu faraja atoa, kutapoa kuchakaa,*
*Mungu aliyemleta, ndiye amemchukua.*

*Mungu aliyemleta, ndiye amemchukua,*
*Leila japo kapita, mengi ametufungua,*
*Tutazidi kumteta, yake tukiyachungua,*
*Na sisi vitabu vyetu, vyema vikawa rejea.*

*Na sisi vitabu vyema, vyema vikawa rejea,*
*Watu wanapovisoma, iwe njia kutokea,*
*Yale kwao yanagoma, wapate pa kupenyea,*
*Amemaliza Leila, kaacha mambo mazito.*

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0a767223602**



## Wajumbe TSC wajengewa uelewa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendesha mafunzo ya Kamati ya Ukaguzi wa ndani ya Tume hiyo ili kuwajengea uelewa wajumbe wa kamati hiyo, Menejimenti na Maafisa Bajeti wa Tume, masuala ya ukaguzi mfumo wa ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za ukaguzi na vihatarishi.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo jijini Dodoma, Katibu wa TSC, Paulina Mkwama alisema, Tume hiyo imeamua kuandaa mafunzo hayo kwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi pamoja na watumishi wengine ili wawajibike kwa kuzingatia sheria na kanuni.

Aidha, Kamati ya Ukaguzi wa ndani ina jukumu la kuhakikisha kuwa shughuli za ndani za taasisi zinafanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia sheria na kanuni.

Alisema ushauri unaotolewa na Kamati hiyo, unafanyiwa kazi jambo ambalo limesaidia TSC kupata mafanikio mbalimbali.

Miongoni mwa mafanikio aliyoyataja ni pamoja na kupata hati safi, kuendelea kuimarishwa kwa Sehemu ya Ukaguzi kabla ya malipo (Pre Audit Section), kuandaliwa kwa mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi (Risk Management Framework), kulingana na Mpango Mkakati wa Taasisi 2021/22 hadi 2025/26 ambao uliwezesha kuandaliwa kwa Daftari la Vihatarishi la Taasisi (Risk Register); na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kuongezewa mtumishi.

Mkwama alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutokana na jitihada zake za kuboresha sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na kutafuta wadau wa maendeleo ili kuendeleza miradi ya elimu, kuajiri na kupandisha madaraja walimu.

"Sote tumeshuhudia ujenzi wa madarasa kuanzia elimu ya awali, msingi na sekondari nchi nzima, kupitia Sera ya Elimu bila malipo, serikali imejenga madarasa 3,000 kwa shule za msingi," alisema.

# Taasisi za umma zatakiwa kuendesha vikao kimtandao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI za umma nchini zimetakiwa kuendesha vikao kidijitali kwa kutumia mfumo wa e-mikutano ili kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao.

Meneja Mawasiliano Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Subira Kaswaga, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu faida zitokanazo na mfumo wa e-mikutano.

Alisema, mfumo wa e-mikutano unawawezesha watumishi wa taasisi hizo kufanya vikao kidijitali mahali walipo bila kulazimika kukutana mahali pamoja na kusaidia kupunguza gharama za uandaaji na uendeshaji wa vikao.

**Mfumo huu wa e-mikutano unazisaidia taasisi za umma kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao.**

"Mfumo huu wa e-mikutano unazisaidia taasisi za umma kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao, watumishi hawalazimiki kusafiri na kukutana mahali pamoja ili kufanya vikao na badala yake wanaweza kufanya vikao mahali walipo," alisisitiza.

Alisema mfumo wa e-mikutano huokoa muda ambao watumishi wangeutumia kusafiri kutoka eneo moja kwenda jingine kwa ajili ya kufanya vikao na kutumia muda huo kutekeleza majukumu yao mengine ili kuongeza ufanisi.

"Mfumo huu pia unasaidia kupunguza au kuondoa kabisa gharama za kulipia leseni zinazohitajika ili taasisi za umma ziweze kutumia mifumo ya uendeshaji wa vikao kidijitali iliyojengwa na kampuni binafsi," alifafanua.

Alisema, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilitengeneza mfumo wa e-mikutano, baada ya kuona uhitaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA kwenye eneo la kuratibu mikutano kwa watumishi wanaokuwa katika mazingira tofauti.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (kulia), akijadiliana jambo na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanaokiuka michakato zabuni za umma kukiona

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), imesema haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa wanaokiuka michakato ya zabuni za umma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Ukidhi wa PPRA, Mhandisi Awadhi Suluo, alisema baadhi ya wazabuni wanaopata tuzo za zabuni za umma wanashindwa kutekeleza matakwa ya mikataba wanayoingia na taasisi za umma na wakati mwingine kushindwa kutokea wakati wa ufungaji wa mikataba yao.

Aidha, alisema hatua zitakazochukuliwa dhidi yao ni kufungiwa kushiriki zabuni za umma.

Alisema wazabuni wengine wanashindwa kutekeleza mikataba yao kwa kutowasilisha bidhaa au kutoa huduma iliyokusudiwa kwa visingizio mbalimbali.

"Kwa mfano kuna mzabuni mmoja (jina limehifadhiwa) alishinda tuzo ya kusambaza bidhaa katika moja ya ofisi za serikali, lakini baada ya kutangazwa hakutokea kusaini mkataba na anatoa visingizio mbalimbali ikiwamo bidhaa hiyo kupanda bei," alisema.

Kadhalika, alisema kitendo cha wazabuni kutosimamia tuzo wanazopewa kupitia zabuni za umma, inazigharimu taasisi za ununuzi kwa kuwasababishia kutumia muda na gharama nyingine za kutangaza zabuni upya na kurudisha nyuma mchakato wa kupata mzabuni mwingine.

"Sheria ya Ununzi wa Umma, kifungu cha 62 (3) (c) sura ya 410 toleo la mwaka 2022, sambamba na ya kanuni za ununuzi wa umma zinaeleza kuwa mzabuni kushindwa kuwasilisha zabuni kwa mujibu wa mkataba kunamtia hatiani kwa kufungiwa kushiriki zabuni za umma kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano," alisema.

## Waonywa kumaliza kesi ukatili kienyeji

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

SERIKALI imewataka wazazi na walezi kuacha tabia ya kumaliza kesi za ukatili wa kijinsia wanazofanyiwa watoto wao kwa njia za kienyeji badala yake watoe ushirikiano ikiwemo kutoa ushahidi kwenye vyombo vya kisheria ili haki kutendeka.

Pia, mashauri yanayofunguliwa yanayohusu ukatili dhidi ya watoto yasiishie kwa kumalizana kifamilia na kindugu na kuwataka wazazi kuyapeleka kwenye vyombo vya kisheria ili haki itendeke na watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo wapate haki zao.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Watoto - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mathias Haule, alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye maadhimisho ya siku Mtoto wa Afrika iliyofanyika katika Kijiji cha Chamwino Ikulu, jijini hapa.

Haule aliyemwakilisha Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwanjima, alisema bado kuna tatizo la baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto wanaofanyiwa vitendo vya kikatili kumalizana kienyeji, kindugu na kifamilia huku wakitambua kuwa kitendo hicho kinaongeza ukatili dhidi ya mtoto.

Aliwataka wazazi hao kutoa ushirikiano kwa uaminifu wanapohitajika kutoa ushahidi kwenye vyombo hivyo vya kisheria, badala ya kuiachia serikali peke yake, ambayo mara nyingi inashindwa kutoa uamuzi sahihi.

"Niwaombe wazazi wezangu tushirikiane na vyombo vya dola vitendo vya kikatili vinapotokea ndani ya familia, iwe vimefanywa na ndugu au watu wengine tuwe tayari kuvifikisha kwenye vyombo vya kisheria na sio kukaa na kumalizana kienyeji au kindugu," alisisitiza.

Mwenyekiti Idara ya maadili na uongozi (SMAUJATA) Mkoa wa Dodoma, Happiness Mgongo alisema, jukumu la ulinzi kwa watoto lipo kwa wazazi na walezi zaidi na kutakiwa kuwajibika kuwalinda na kupatiwa haki zote za msingi.





# Wakulima kahawa waomba mfumo wa tozo ubadilishwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa kahawa wa Kanda ya Mbeya inayojumuisha mikoa ya Songwe, Rukwa na Mbeya wameiomba serikali kubadili mfumo wa kukusanya tozo ya maendeleo ya zao hilo kutoka Sh. 200 kwenye kila kilo moja ya kahawa badala yake ikusanywe kwa viwango vya asilimia.

Wakizungumza jana kwenye kikao cha wadau wa kahawa wa kanda hiyo kilichofanyika jana jijini hapa, baadhi ya wakulima hao walisema kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya bei wakati mwingine tozo ya Sh. 200 kwa kila kilo ya kahawa inamuumiza mkulima.

Benjamin Mwambungu, mkulima wa kahawa kutoka Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe alisema ipo haja kwa serikali kupitia bodi ya kahawa kupitia upya tozo hiyo na kuamua kupanga viwango vya tozo kwa mtindo wa asilimia ili kutomuumiza mkulima.

"Wakati tozo ya Sh. 200 inapangwa, bei ya kahawa aina ya arabika ilikuwa Sh. 6,000 kwa kilo, kama ingeendelea kuwa bei hiyo mpaka mwisho wa msimu isingekuwa shida, lakini bei hushuka hadi kufikia Sh. 4,000 kwa kilo huku tozo ikibakia kuwa Sh. 200 jambo ambalo sasa linageuka kuwa maumivu kwa wakulima.

**Wakati tozo ya Sh. 200 inapangwa, bei ya kahawa aina ya arabika ilikuwa Sh. 6,000 kwa kilo, kama ingeendelea kuwa bei hiyo mpaka mwisho wa msimu isingekuwa shida...**

"Sisi wakulima tunapendekeza tozo hii ikusanywe kwa mtindo wa asilimia ili kama bei ikiongezeka na tozo nayo inaongezeka na ikishuka pia inapungua jambo ambalo litatoa unafuu kwa mkulima, lakini na kuihakikishia serikali mapato yake," alisema Mwambungu.

Daudi Simkoko, mkulima wa kahawa kutoka Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe alisema bei ya kahawa wakati mwingine inatofautiana kutoka mkoa mmoja na mwingine, lakini wote wanatozwa kiwango sawa cha tozo, hali ambayo inawaumiza baadhi ya wakulima, mfumo wa kutozwa kwa asilimia utaleta usawa kwa wakulima wa zao hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Kajiru Kisenge, alisema watayafanyia kazi maoni hayo huku akibainisha kuwa tozo hizo zina manufaa makubwa katika uendelezaji wa zao la kahawa kwa kuwa zinatumika kutatua changamoto nyingi zinazowakabili wakulima wa zao hilo.

"Kwa msimu uliopita fedha hizo zimetumika kuzalisha miche ya kahawa na kusambaza kwa wakulima na kupunguza kero ya muda mrefu ya ukosefu wa miche ya kahawa na endapo tozo hiyo itaendelea kukusanywa ipasavyo, inakusudiwa kutumika kujenga mabwawa yatakayotumiwa na wakulima kumwagilia mikahawa yao wakati wa ukame," alisema Kisenge.

Akiongoza kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliitaka Bodi ya Kahawa kushughulikia kero walizonazo wakulima ili zao hilo liwe na tija kwa kuwa mikoa hiyo mitatu inazalisha zaidi ya asilimia 54 ya kahawa yote inayozalishwa nchini na kuchangia pato la taifa.



Meneja wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Jasper Samwel (kushoto), akitoa maelezo kwa wahariri na waandishi wa vyombo vya habari nchini, waliotembelea kituo kikuu cha hifadhi ya nafaka cha kanda hiyo, kinachozalisha bidhaa ya unga wa mahindi na kinachosimamiwa na CPB, mjini Iringa juzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Idadi kubwa waendesha bodaboda ni watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDADI kubwa ya waendesha bajaji na bodaboda mkoani hapa ni vijana wenye umri ulio chini kisheria na wasio na mafunzo ya usalama barabarani, hali inayosababisha ongezeko la ajali za barabarani.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alipozungumza na kundi hilo kuwa ili kukabiliana na wimbi la watoto kuendesha bodaboda na bajaji, aliagiza Kikosi cha Usalama barabarani kuanza operesheni ya kukagua leseni za madereva kukabiliana na wimbi la watoto hao ambao wamekuwa wakisababisha ajali na misongamano barabarani.

"Tumefanya uchunguzi na kubaini idadi kubwa ya watoto kuendesha bajaji na bodaboda, hasa nyakati za usiku, jambo ambalo ni kinyume na sheria za usalama barabarani, naomba Jeshi la Polisi muanze operesheni ya kukagua leseni kuangalia ukubwa wa tatizo hili ambalo linasababisha ongezeko la ajali mkoani hapa," alisema Malisa.

Alitaka ukaguzi wa leseni uanze mara moja kuanzia majira ya saa 12 jioni ili kuwakamata watoto ambao wamejiingiza kwenye udereva bila leseni hali inayohatarisha maisha ya watumiaji wengine wa barabara.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama barabarani, Mkoa wa Mbeya, Yusuph Kamotta, alisema chanzo kikubwa cha ajali mkoani humo ni makosa ya kibinadamu huku akibainisha vyanzo vingine kuwa ni ubovu wa magari na kuwasihi madereva kutokubali kuendesha vyombo vya moto vibovu hata kama wanalazimishwa na mabosi zao badala yake watoe taarifa za siri kwa Polisi ili kuyakamata magari ya namna hiyo.

Kamotta aliomba serikali kuanzisha mtaala kuhusu usalama barabarani kuanzia shule za msingi ili kujenga uelewa kwa vijana na kuwaandaa kukabiliana vikwazo vinavyotokea barabarani.

# TGNP yazishauri halmashauri kupanga bajeti zao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umezishauri halmashauri nchini kupanga mipango ya bajeti zao inayojielekeza katika kutatua vikwazo vya masuala ya kijinsia ili kuendana na malengo ya mpango wa maendeleo endelevu ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Programu na mafunzo kutoka TGNP, Anna Sangai, alipotoa mafunzo kwa madiwani, wataalamu wa idara ya elimu na afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, yaliyolenga kuwajengea uwezo ili waweze kuandaa bajeti kwa kuzingatia mrengo wa kijinsia.

Anna alisema sera za nchi zinatambua umuhimu wa masuala ya kijinsia hususani wanawake ambao wana mahitaji tofauti yanayosababisha kupata vikwazo mbalimbali zikiwamo za kiafya na kielimu na kwamba ni muhimu kuwapo na bajeti zinazoangalia mahitaji ya kijinsi ili kukabiliana nazo.

"Kama mnavofahamu Tanzania kama zilivyo nchi nyingine tumeridhia mikataba mingi ya kikanda na kimataifa ambayo inatuelekeza kufanya shughuli zitakazohamasisha masuala ya usawa wa kijinsia, sasa tusipokuwa na bajeti ambayo inaelekeza kushughulikia itakuwa ni vigumu kwetu kufikia usawa wa kijinsia," alisema Sangai.

Deogratias Temba, alisema uwapo wa bajeti ambayo inagusa masuala yenye mrengo wa kijinsia unaonesha halmshauri husika ina utashi wa kisiasa jambo ambalo litasaidia wadau wengine ukiwamo mtandao huo kusaidia halmashauri hizo.

Temba alisema ikiwa bajeti zilizopangwa zitazingatia masuala ya kijinsia na kutekelezwa ipasavyo, zitatatua matatizo mbalimbali kwenye sekta ya elimu na afya na kusababisha watoto wa kike kutoyafikia malengo yao.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Halmashauri ya Mbeya, Agnes Elikunda, alisema mafunzo hayo yamewasaidia namna ya bora ya kutenga bajeti kwa kuzingatia jinsia na kuwasaidia kuboresha bajeti zao katika utekelezaji wa masuala ya kijinsia katika maeneo mbalimbali ikiwamo elimu.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Emiliana Mbise, alisema jamii imekuwa na mwamko wa kutoa taarifa ya matukio ya ukatili, lakini vikwazo wanayokabiliana navyo ni kukosa ushahidi kutoka kwa mwathirika na watu wa karibu na kusababisha kutopatikana kwa haki.



# ACT: Umoja, mshikamano utatoa haki Katiba mpya

Na Mwandishi Wetu

MSHAURI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mansor Yussuf Himid, amesema malengo ya Zanzibar kuwa na mamlaka kamili hayawezi kufikiwa bila ya kuwa na umoja na mshikamano katika mchakato wa Katiba ya Muungano ulioanzishwa tena na Rais Samia Suluhu Hassan.

Mansour aliyasema hayo jana wakati akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Tumbe Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Alisema Wazanzibari hawapaswi kukata tamaa kupigania fursa na haki za Zanzibar ndani ya Muungano kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo ili Zanzibar isimame kiuchumi na kujitegemea.

"Bunge la Katiba linakuja, tuanze mapema kushikamana maana wazanzibari tupo kama yatima, lazima tusimame wenyewe kudai Katiba mpya," alisema Mansour.

Alisema mfumo wa Muungano wa sasa una matatizo mengi na unaibana Zanzibar kiuchumi kwa sababu haina fursa ya kukopa katika taasisi za fedha za kimataifa au fedha za ujenzi wa bandari.

Alisema Chama cha ACT kinataka Zanzibar iwe na mamlaka kamili kama ilivyokuwa kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar jambo litakaloharakisha maendeleo kwa maslahi ya wananchi wake.

Alisema misingi ya marehemu Seif Sharif Hamad, itaendelea kuwa imara chini ya uongozi wa chama hicho na kuwataka wananchi kutokata tamaa kutafuta mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi Zanzibar.

Alisema Chama cha Wananchi (CUF), kilipandikiziwa mgogoro wakiamini kuwa kikifa ndiyo mwisho wa upinzani, badala yake wameongeza kasi ya kudai mabadiliko kwa wananchi kupitia kauli ya Maalim Seif, shusha tanga, patisha tanga, safari inaendelea.

Hata hivyo, alisema wanachama wa ACT wanahitaji kusimama imara kuelekea uchaguzi wa mwaka 2025 ili chama kufikia malengo ikiwamo kuleta mabadiliko ya utawala visiwani Zanzibar.

"Sisi hatuna jeshi, polisi wala vikosi, lakini tutaendelea kupaza sauti kuona haki inatendeka katika mfumo wa demokrasia kuelekea uchaguzi mkuu," alisema Mansour.

Aidha, alisema CCM imeshindwa kulinda misingi ya Mapinduzi kutokana na vitendo vya ubaguzi vinavyoendelea kujitokeza kwa sababu ya itikadi za kisiasa na kuteteresha umoja wa kitaifa kwa wananchi wa Zanzibar.

Katika mkutano huo, Mansour alitoa siri watu waliokuwa wakijua mrithi wa Maalim Seif kabla ya kufariki ni watu wawili akiwamo yeye na Ismail Jussa, na yeye ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kumuita ofisini na kumueleza wakati wake umemalizika wa kugombea na kutaja mrithi wake ni Othman Masoud.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alisema Zanzibar ilikuwa ni dola inayotambulika duniani kabla ya kuzaliwa Jamhuri ya Tanganyika, mwaka 1937.

Alisema, Zanzibar ilijiunga na Umoja wa Mataifa, mwaka 1963 ikiwa na mamlaka kamili na mipaka ya nchi yake ni kisiwa cha Unguja na Pemba pamoja na kisiwa cha Fungu Mbaraka.

Othman ambaye amewahi kuwa Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar (DPP), alisema bahati nzuri nyaraka zote zipo na kuwataka wananchi kuondoa wasiwasi, cha muhimu ni kujenga umoja na mshikamano kuelekea katika mchakato wa Katiba ya Muungano ili Zanzibar ilinde rasilimali zake.

Aidha, alisema kimsingi Zanzibar haina uwezo wa kuchimba mafuta na gesi baada ya jambo hilo kuongezewa katika orodha ya mambo ya Muungano na mipaka ya nchi na ardhi kupotea baada ya Mapinduzi ya Januari ya mwaka 1964.

"Mambo ya Muungano yalikuwa 11, lakini yakaanza kuoengezwa kinyemela, wakaingiza suala la bandari, kodi, mafuta, lakini nyaraka zote za mambo ya Muungano zipo ndiyo maana tunataka Zanzibar iwe na mamlaka kamili kulinda rasilimali zake," alisema.

Alisema kisiwa cha Shelisheli ni kidogo kuliko Zanzibar, lakini kimepiga hatua kubwa kwa sababu kina mamlaka kamili na kuwata viongozi na wananchi kuacha kutetea maslahi binafsi kuelekea mchakato wa Katiba.

Awali, mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema wananchi wa Pemba ni walimu wa siasa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Alisema ni watu wanaosimama imara kupigania mabadiliko ya kisiasa na kiutawala licha ya misukosuko inayowakuta kwa maslahi ya Zanzibar.

Alisema wakati wa kuelekea mjadala wa Katiba ya Muungano, kazi kubwa iliyopo mbele ni kuipapatua Zanzibar katika muungano wa serikali mbili ili kuwa dola kamili na kiti chake Umoja wa Mataifa.

# ZATUC yandaa mchakato sera kusimamia w'kazi sekta zisizo rasmi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Vyama Vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), limo katika mchakato wa kuandaa sera ya sekta zisizorasmi ili kuwa na sera ambayo inawasimamia wafanyakazi wa sekta hiyo na kupata haki zao zote mfanyakazi anastahili kuzipata.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa, Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano, Uchukuzi na usafirishaji Zanzibar (COTWU ZNZ), Amour Mussa Makame, alisema sekta hiyo ni muhimu na imewekeza watu wengi katika nchi wakiwamo asilimia 85 ya wananchi wa Zanzibar kuwekeza katika eneo hilo.

Alisema, ni lazima wahakikishe wanasaidiwa na msaidizi mkubwa ni vyama vya wafanyakazi.

Hata hivyo, alisema sekta zisizo rasmi zinahitaji kusimamiwa ili shughuli wanazozifanya ziwaletee faida na utaratibu unaokubalika, hasa mchango mkubwa katika pato la nchi na wanalipa ushuru.

"Sekta isiyo rasmi inajiona ni eneo lililojitenga, lakini sio hivyo, bali ni sekta ambayo inazalisha na inatoa pato kubwa katika nchi, inatoa michango na kulipa ushuru na mambo mingine," alisema.

Aidha, alisema sekta iliyo rasmi ina sheria ambazo zinawalinda katika utendaji wa shughuli zao za kazi za kila siku ikiwamo sheria ya ajira, ya usalama wa afya kazini, ya fidia na sheria namba mbili ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), vitu ambavyo vinakosekana katika sekta isiyo rasmi.

Alisema, wapo kwenye mchakato wa kuhakikisha kwamba watafika siku kuiomba serikali inawatengenezea sera sekta hiyo ili kujikomboa katika masuala mbalimbali.

Makame alisema wao wakiwa ni watetezi wakuu wa wafanyakazi kupitia vyama vyao, sasa hivi wanapambana kuhakikisha sera ya sekta isiyo rasmi Zanzibar inapatikana, na uwapo wa sera hiyo itawatetea na itawastawisha kuhakikisha madai na malalamiko pamoja na changamoto zinazowakumba wafanyakazi wa sekta hiyo zinaelezwa.

Aidha, alisema sekta isiyo rasmi inahitaji kujengewa hifadhi ya jamii, kupata haki za kijamii kuhakikisha vitu vinakuwapo na wao wanakuwa navyo.

**Sekta isiyo rasmi inajiona ni eneo lililojitenga, lakini sio hivyo, bali ni sekta ambayo inazalisha na inatoa pato kubwa katika nchi, inatoa michango na kulipa ushuru na mambo mingine.**




Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Benki ya Biashara (TCB), Gloria Mutta (kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa vya watoto wenye mahitaji maalum kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Jeshi la Wokovu, Mary Raphael Nyika Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu mpango wa benki hiyo katika kuwajibika kwa jamii (CSR). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZMA yasajili zaidi ya meli 400 kuongeza mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA), imefanikiwa kusajili jumla ya meli 419 zenye uzito wa GT 1,922,14864 kwa meli za nje huku jumla ya meli 29 za ndani zimesajiliwa katika kipindi cha mwaka 2020-2023.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu waziri wa wizara hiyo, Nadir Abdillatif Yussuf, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe, aliyetaka kujua maendeleo ya ZMA kwa sasa.

Alisema, inaendelea kufanya vizuri katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwamo kutangaza shughuli zake nje ya nchi.

Pia, mafanikio hayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mapato katika taasisi hiyo pamoja na uchumi wa Zanzibar.

Aidha, wamejipanga kikamilifu kutokana na mwenendo wa meli zote zilizopewa usajili wa kudumu kuona zinazingatia masharti ambayo yanawafanya kupeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimataifa.

"Tumejipanga vizuri kuona kwamba meli zote zinazopeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano zinafuata masharti ikiwamo kuepuka kufanya vitendo vinavyokwenda kinyume na madili yetu," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASPOTI YA KUSAFIRIA



**AMIRI RAMADHANI MHINI** anatangaza kupotea kwa paspoti ya kusafiria yenye namba **TAE 290849** iliyotolewa **DAR ES SALAAM PCO 29** Januari, **2020.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**TAARIFA POLISI: DAR/TAB/RB/190079/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SETI ERIA NSOHOYE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1660-0054** kilichotolewa na **MKOZA SEKONDARI** mwaka 2015. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1611-0054** kilichotolewa na **KALENGE SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **KIG/BUH/RB/326342/2022 / KIG/BUH/RB/326368/2022.**

NACTE REG. NO: REG/HAS/289
STATUS: FULL ACCREDITATION

MKOLANI FOUNDATION HEALTH SCIENCES TRAINING INSTITUTE

## KUMRADHI

Uongozi wa Chuo cha Afya Mkolani unaomba radhi kwa Umma kwa tarehe iliyokuwa imeandikwa kwenye ujumbe mfupi uliotumwa kwa waombaji wa kujiunga na masomo mwaka huu. Hivyo tunapenda kutarifu umma kuwa tarehe ya kufungua chuo ni tarehe sawa na ile itakayotangazwa na baraza la taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZNIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha KIHONDA**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 62/2023**
**Jina la Mdai: JOSEPH KAWICHE**
**Jina la mdaiwa: NEEMA TEMU (NANE NANE AGROVET)**

### KUITWASHAURINI

(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu za madai katika mahakama za mwanzo)

**Kwa: NEEMA TEMU (NANE NANE AGROVET) WA KIBAHA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za mdai) **MADAI YA PESA YA TSHS. 6000,000/=.**

Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 19 mwezi wa 06 mwaka 2023 Saa.....Asubuhi / Mchana kwa mujibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitikwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mhakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe13 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**
**MAOMBI MADOGO Na. 192 YA 2023.**
**EMMANUEL BENJAMINI KIULA............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**KAWEDI MAKYAO......... MJIBU MAOMBI**

### WITO WA KUITWA MAHAKAMANI

**KWA:KAWEDI MAKYAO**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ombi dhidi yako katika baraza la Ardhi na nyumba mkoa wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 22/06/2023 katika chumba cha baraza Na. 3, jengo liko mkabala na mahakama ya mwanzo mjini na mahakama ya wilaya ya nyamagana.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila ya wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya Baraza leo Tarehe 13/06/2023.

MURIRYA N.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo KIHONDA**
**Wilaya ya MOROGORO**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 37 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**YASSINI MUSA MBAGA wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA YAHAYA MUSSA MMBAGA**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **20** Mwezi **06** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe **13** mwezi **06** mwaka **2023**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NASSOR RAJAB DACHI** anatangaza kupotelewa kadi ya gari yenye namba za usajili **T994 DHD** aina ya Townace Noah. Chassis namba **SR400124940** na Engine namba **3S5053195**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MAN/BAB/RB/200852/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHEBEKI STEWADI NGUNGANYI** mkazi wa Shinyanga anatangaza kupotelewa Kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** Namba **MC 938 CTQ.** Taarifa hii imeripotiwa Kituo cha Polisi Shinyanga.

Yeyote atakayeiona Kadi ya Pikipiki yenye Namba hiyo atoe taarifa Kituo cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi:
**SHI/SHI/RB/194194/2023.**

**FORM NO. 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 541 OF 2023**
**In Matter of Estate of the Late**
**CHARITY BATULI KASUBI**
**and**
**In Matter of Application for letters of administration by**
**VICTOR SERY KESSY**

### GENERAL CITATION

**(Rule 75)**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latters of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grand should be field on or before the **17** day of **07, 2023**

Dated at **DAR ES SALAAM**, this **30** day of **05, 2023**

Senior Resident Magistrate

*OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

KESI WIZI WA GARI

# Askari amshtua hakimu kutoa ushahidi upande wa mshtakiwa

Na Grace Gurisha

SAKATA la wizi wa gari aina ya RAV4 lenye namba za usajili T. 984 BPG, limeendelea kuibua mapya katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, baada ya askari polisi J 212 PC Damas kutoka Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni kutoa ushahidi akiwa upande wa mshtakiwa.

Wakati Damas anatoa ushahidi wake kwa kumtetea mshtakiwa Salum Mshana, tayari baadhi ya askari, akiwamo mpelelezi wa kesi hiyo walishatoa ushahidi wao kwa upande wa mashtaka kwa lengo la kuthibitisha wizi wa gari hilo.

Hali hiyo ilitokea juzi mbele ya Hakimu Mkazi, Aaron Lyamuya wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya usikilizwaji wa mashahidi wa upande wa mashtaka, ndipo askari huyo alipopanda katika kizimba cha shahidi.

"Sijawahi kukutana na kitu kama hiki - polisi kuja kuzungumza kwa upande wa utetezi. Siyo kusema kwamba inakatazwa, hapana! Inaruhusiwa kabisa.

"Haya, sawa ngoja tumsikilize. Sasa sijui utazungumza nini wakati wenzako walishazungumza kwa upande wa mashtaka. Haya mwapishe tuanze," alisema Hakimu Lyamuya.

Akitoa ushahidi wake, akiongozwa na Wakili wa Mshtakiwa, Constantine Kakula, Damas alidai kuwa yeye anatoka ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Kitengo cha Masijala Dawati la Malalamiko.

Alidai kuwa kabla ya Aprili 17 mwaka huu, walipokea barua ya malalamiko kutoka kwa Salum ikieleza kuwa kuna mtu anatumia gari hilo wakati siyo lake. Wakaanza kulifanyia kazi kwa kuandika barua Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Tuliandika barua TRA ili kujua nani mmiliki wa gari hili. Majibu yalirudi kwamba mmiliki wa awali ni Victoria Njau na wa sasa ni Clerance, jina lake la pili nimelisahau kidogo.

"Baada ya taarifa hizo, tulianza kuchunguza Clerance anaishi wapi. Tulibaini anaishi Goba, Dar es Salaam. Tulikwenda kwake tukajitambulisha kuwa sisi ni maofisa wa polisi, tukamwuliza 'kuna gari ambalo unatumia sio lako?' Akajibu ni kweli," alidai Damas.


Baada ya taarifa hiyo, Damas alidai waliondoka na Clerance pamoja na gari hilo lenye namba za usajili T 984 BPG hadi Kituo cha Polisi Oysterbay.

"Nilitaka kuja nalo hapa lakini ni bovu, lilishindwa kuwaka, ila nikipewa muda nitalileta," alidai.

Hakimu Lyamula alimweleza kwamba kabla ya siku ya Ijumaa, awe amelifikisha gari hilo kwenye viwanja vya mahakama ili Jumatatu wakati wa usikilizwaji wa shauri hilo liwapo kwa ajili ya kuliangalia kama ndiyo alilolielezea mbele ya mahakama ndipo aombe litolewe kama kielelezo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Juni 19 mwaka huu kwa kuendelea kusikilizwa. Gari analodaiwa mshtakiwa Salum kuwa ameliiba ndiyo alilokutwa nalo Clerance ambapo umiliki ulibadilishwa kutoka kwa Njau kwenda kwa Clerance Oktoba 25, 2022.

Katika hati ya mashtaka, mfanyabiashara huyo anatuhumiwa kuwa Oktoba 21, 2015, akiwa eneo la Ubungo External, aliiba gari aina ya RAV4 T 984 BPG, mali ya Victoria Njau ambalo alikuwa ameaminiwa na Peter Sanga kwa ajili ya biashara.



Watuhumiwa wa kesi ya kukutwa na vipande 660 vya meno ya tembo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4 (mstari wa mbele), wakiwa katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza shauri linalowakabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Kesi ya vipande 660 vya meno ya tembo yakwama

Na Kulwa Mzee

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili raia wa Guinea, Ally Angozuu na wenzake wanaodaiwa kukamatwa na vipande 660 vya meno ya tembo, imekwama kuendelea kusikilizwa kutokana na baadhi ya mawakili wa washtakiwa kutofika mahakamani.

Shauri hilo lilitakiwa kuendelea jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mrio.

Upande wa Jamhuri katika shauri hilo ukiwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Hemed Halfan, ulidai una shahidi mmoja kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Wakili huyo alidai mahakamani kwamba baadhi ya mawakili wa utetezi, akiwamo Nehemia Nkoko anayemwakilisha Angozuu, hawakuwapo mahakamani, hivyo aliiomba mahakama kuahirisha kesi hiyo.

Washtakiwa walipotakiwa kutoa taarifa za mawakili wao, walieleza sababu mbalimbali huku baadhi yao wakidai hawana taarifa zao.

Washtakiwa waliomba mahakama iendelee kusikiliza ushahidi wa kesi hiyo hata kama mawakili wao hawapo.

"Mheshimiwa hatuwezi kuendelea na kesi kwa sababu mawakili wa washtakiwa hawapo, kufanya hivyo ni sawa na kutengeneza hoja za rufani, sisi itatupa shida huko mbele. Kama wanataka tuendelee, wakubali kuwaondoa mawakili wao wawe hawana uwakilishi," alidai Halfan.

Hakimu aliwahoji washtakiwa hao kama wako tayari kuwaondoa mawakili wao, walikataa na kusisitiza kuwa wako tayari kuendelea na kesi bila mawakili wao kuwapo na watakapokuja, wataendelea kuwawakilisha.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 22 mwaka huu kwa ajili ya usikilizwaji huku akiwataka washtakiwa kuwataarifu mawakili wao wawapo mahakamani tarehe hiyo ya kesi.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Victor Mawala, Haruni Abdallah, Abbas Hassan, Solomoni Mtenya, Khalfani Kahengele, Ismail Kassa, Juma Buguma, Kassim Saidi, Peter Nyachiwa, John Buhanza na Mussa Abdallah, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Katika shauri hilo, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, ambazo ni vipande hivyo vya meno ya tembo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa na mtandao mkubwa wa uhalifu wa ujangili ambao unajihisisha na kuuza, kununua, kupokea na kuhamisha, kusafirisha nyara za serikali ambazo ni meno ya tembo.

## Wazindua huduma kuwezesha watanzania kusoma

Na Frank Monyo

KAMPUNI ya Mawasiliano ya Vodacom Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya SILABU wamezindua huduma itakayowarahisishia watanzania kujifunza masomo na taaluma mbalimbali kwa ngazi tofauti kwa njia ya mtandao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo uliofanyika katika Ofisi za Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) mkoani Dar es Salaam, Kamishna wa Elimu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alipongeza jitihada za Vodacom na SILABU kwa ubunifu wa huduma ya kujifunza mtandaoni inayoendana na mahitaji ya soko la elimu nchini na duniani kote kwa sasa.

"Elimu ya sasa haitulazimishi kuwapo moja kwa moja darasani ili tuweze kujifunza. Kuwapo nyenzo za kidigitali kunarahisishia wanafunzi na watu wa taaluma mbalimbali kujisomea na kujifunza kwa njia ya mtandao.

"Ongezeko la vifaa vya kidijiti kama simu janja, kompyuta na vishkwambi na miundominu ya intaneti vinaendelea kuwa chachu ya mapinduzi ya kidijitali katika sekta ya elimu.

"Niipongeze Vodacom kwa hatua hii kwani nimefahamishwa kuwa SILABU ni matokeo ya programu ya 'Vodacom Digital Accelerator', ambayo huzisaidia kampuni changa za kibunifu zinazotumia teknolojia kutatua changamoto zinazoikumba jamii yetu ya Watanzania," alisema.

Dk. Mtahabwa aliongeza "…ningependa kutoa rai kwa wanafunzi na Watanzania wote kutumia vyema majukwaa haya ya kidigitali kujisomea na kujifunza masomo mbalimbali ambayo mengine hayapatikani darasani."

Mkurugenzi wa Huduma za Kidigitali wa Vodacom Tanzania PLC, Nguvu Kamando, alisema SILABU ni uthibitisho tosha kuwa vijana wa kitanzania wana bunifu wenye tija na wanaweza kufika mbali endapo wakipewa fursa na hamasa ya kuzitekeleza.

"SILABU ni mojawapo ya matunda kutoka kwenye programu yetu ya Vodacom Digital Accelerator (VDA) ambapo tunazishindanisha kampuni changa bunifu zinazotumia teknolojia kuleta mageuzi katika sekta ya elimu, afya, kilimo, usafiri, fedha na biashara za mtandaoni," alisema.

Ofisa Mkuu Uendeshaji wa SILABU Tanzania, Adam Duma, alisema "…SILABU inatoa wigo mpana wa kujifunza kupitia madarasa yenye masomo yanayokidhi mahitaji ya ngazi tofauti za elimu kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari, chuo kikuu pamoja na kozi zinazomwezesha mtu kujiongezea ujuzi na maarifa."

# FOUNTAIN GATE YAINUNUA RASMI SINGIDA BIG STARS

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa taasisi ya kukuza vipaji vya soka ya Fountain Gate Academy Tanzania, imetangaza kuinunua timu ya Singida Big Stars inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na sasa itaitwa Singida Fountain Gate huku makazi yake yakiendelea kuwepo mkoani Singida.

Singida Big Stars msimu uliofikia tamati mwishoni mwa wiki ilimaliza katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 55 na imekata tiketi ya kushiriki michuano ya kombe la Shirikisho Afrika (CAF) kwa msimu 2023/24.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Taasisi za Fountain Gate Academy Tanzania, Japhet Makau alisema uamuzi wa kuichukua timu hiyo ni kutoa fursa kwa vijana kuweza kuonekana kwa sababu Taasisi hiyo ina timu za Fountain Gate FC zinazocheza ligi za madaraja mbalimbali zinazotambulika na Shirikisho la Mpira wa miguu Tanzania, TFF.

Alisema kumiliki kwa timu hiyo kutawapa nafasi wachezaji wa timu hizo za chini kuweza kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha timu kubwa ya Singida Fountain Gate.

"Kuinunua timu ya Singida Fountain Gate katika ligi itawapa nafasi wachezaji kutoka katika kituo chatu na timu kutoka ligi daraja la kwanza kupata nafasi ya kucheza ligi Kuu na kucheza michuano ya kimataifa," alisema Makau.

"Tumeichukua timu hii na itaendelea kubaki Singida, kwa kuwa Singida Fountain Gate FC inashiriki michuano ya kimataifa na CAF wahaitaji timu zote zinazoshiriki michuano hiyo kumilikia timu ya wanawake hali hiyo inayotulazimu timu yetu ya wanawake ya Fountain Gate Princess kuwa Mali ya Singida Fountain Gate," alisema Makau.

Aliongeza kuwa Jukumu la kwanza walinalohitaji ni kuwa na bodi ambayo inaenda kusimamia timu na kufikia malengo wanayotarajia na itaendeshwa kwa mtindo wa bodi ambayo itakuwa wajumbe 9 pamoja na Rais.

"Kwa upande wa Rais nitaendelea kuchukua nafasi hiyo ambayo nimejiuzulu kwenye bodi ya taasisi ya Fountain Gate FC na wajumbe wangu watakuwa John Kadutu, Mbuge wa Singida, Mussa Sima, Festo Sanga (Mbuge wa Makete) na Joseph Msafiri (Mkurugenzi wa shule za Fountain Gate).

"Pia Alexander Mnyeti (Mbuge wa Misungwi), Omary Kiwanda na Ibrahim Mirambo na nafasi mbili zitatangazwa hapo baadae ambao watakamilisha bodi, lakini pia tunamtangaza Mtendaji Mkuu ambaye anatoka nchini Botswana, Olebile Sikwanza," alisema Makau.



Rais wa Taasisi ya Fountain Gate, Japhet Makau (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati akitangaaza kuinunua timu ya Singida Big Stas na kuitwa Singida Fountain Gate FC, katikati ni Mjumbe wa Bodi wa timu hiyo, John Kadutu, na kulia ni Mtendaji Mkuu wa Fountain Gate, Olebile Sikwane. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Julio: KMC tutabaki Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kufungwa mabao 2-1 na ya Mbeya City juzi kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya, Kocha Mkuu wa KMC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema bado wana imani ya kubaki Ligi Kuu, kwani mechi ya marudiano wanakwenda kucheza nyumbani wakiwa na mtaji wa bao moja.

Akizungumza mara baada ya mechi ya kwanza ya 'play off', Julio amesema ilikuwa ngumu kwa sababu kila timu ilitaka ushindi ili kujibusuru kushuka daraja, lakini kitendo cha kupata bao moja kimewafanya wawe na imani kuwa wanaweza kupindua matokeo nyumbani.

"Mechi ilikuwa ngumu, kila timu ilicheza kwa nguvu ikiwa na nia ya kutaka kujinusuru, hili bao moja linaweza kusababisha mimi kufanya vizuri kwenye mechi ya marudiano," alisema Julio.

Akiizungumzia mechi yenyewe alisema kipindi cha kwanza wachezaji wake hawakuwa na utulivu kutokana na presha ya mchezo wenyewe, lakini alipofanya mabadiliko kipindi cha pili, kila kitu kikabadilika.

"Kipindi cha kwanza vijana wangu hawakuwa na utulivu kwa sababu ya presha ya mechi yenyewe, kipindi cha pili nilifanya mabadiliko vijana wangu wakatulia lakini kwa bahati mbaya tumepoteza, tukijipanga vizuri tutabaki Ligi Kuu," alijinasibu.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mbeya City, Abdallah Mubiru alilia na safu yake ya ushambuliaji, akisema kuwa ilitakiwa kufunga mabao mengi.

"Wachezaji wamefanya kila kitu walichoweza na uwezo ndiyo umefikia pale, tumeklosa kufunga magoli tu, kwenye soka ndiyo maana timu kubwa zinakwenda kununua masstraika kwa gharama kubwa, angalia tunacheza vizuri lakini ufungaji ndiyo tatizo, unaweza kufundisha sana mazoezini jinsi ya kufunga, lakini wakati mwingine kuweka mpira ndani ya wavu ni kipaji cha uwezo wa mtu binafsi wa mchezaji," alisema.

Hata hivuo alisema watakwenda kupambana kwenye mechi ya marudiano kuhakikisha wanabaki Ligi Kuu.

Mechi ya pili inatarajiwa kuchezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga ambako KMC imeamua kulipeleka pambano hilo huko.

Mshindi wa jumla atabaki Ligi Kuu na aliyefungwa atakwenda kucheza mechi nyingine ya mchujo dhidi yimu ya Championship ya Mashujaa FC ya Kigoma.

# Azam kuja kivingine msimu ujao

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Azam FC limesema linajipanga kufanya usajili wa kishindo kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti Nipashe jana Kocha wa timu hiyo, Kally Ongala alisema licha ya kukosa taji lolote msimu huu hawajakata tamaa na wanakwenda kujipanga upya.

"Tutakwenda kukiboresha kikosi chetu msimu ujao kwa kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani na si ukubwa wa majina," alisema Ongala.

Kocha huyo alisema msimu uliopita ulikuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa na kuahidi kurekebisha mapungufu yote yaliyojitokeza msimu huu.

Alisema watarudi kivingine msimu ujao na kuomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono ili watimize malengo yao.

"Tunaomba mashabiki wetu wasikatishwe tamaa na matokeo tuliyoyapata msimu huu bali waendeleze ushirikiano msimu ujao, kwani kila kitu kitakaa sawa," alisema.

# Ruvu kubaki na kocha Makata

**Na Abdallah Mataka**

TIMU ya Ruvu Shooting yenye maskani yake Mlandizi Mkoani Pwani imesema haina mpango wa kuachana na kocha wake, Mbwana Makata licha ya kushindwa kuinusuru na janga la kushuka daraja msimu huu.

Akizungumza na Nipashe msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire alisema mara baada ya timu hiyo kushuka daraja na kuelekea championship, bado wanaimani na kocha huyo kuendelea kuwatumikia maafande hao, labda kama ataomba mwenyewe kuondoka.

"Itategemea na kocha mwenyewe kama ataridhia kuondoka au kubaki, lakini sisi hatuna tatizo, akiamua kuondoka tutamruhu," alisema Bwire.

"Ruvu haina tabia ya kumtupia lawama mwalimu inapotea timu imefanya vibaya kwani huwa hatuna kasumba ya kusema mwalimu ndo kasababisha timu kuwa na kiwango kibovu, huwa tuna wigo mpana wa kutafakari mambo mbalimbali na kutafakari wapi tumeteleza na wapi tufanye maboresho ili timu yetu iwe vizuri".

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ATAKIWA MAN

KLABU ya Manchester United itaongoza kinyang'anyiro cha kumnunua fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24 kutoka Paris St-Germain ikiwa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England itanunuliwa na Sheikh Jassim bin Hamad Al Thani. **(Metro)**

### CHELSEA NAO WAJITOSA

CHELSEA pia inatarajiwa kumtaka Kylian Mbappe baada ya mshambuliaji huyo kuwaambia PSG kuwa hataki kuongeza mkataba baada ya mwaka 2024. **(Times)**

### MBAPPE NA REAL MADRID

KLABU ya Real Madrid pia inataka kumsajili Kylian Mbappe msimu huu wa joto, jambo ambalo litaboresha uwezekano wa Tottenham Hotspur kumbakisha mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29 ambaye pia amekuwa akihusishwa na klabu hiyo ya Hispania. **(Mail)**

### SANCHO AWANIWA VILLA

MANCHESTER United iko tayari kumuuza winga wa England, Jadon Sancho, lakini wakati Aston Villa wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hawataki kulipa bei inayotakiwa ya pauni milioni 60. **(Football Transfers)**

### PEPE KUUZWA

KLABU ya Arsenal haina mpango wa kumrejesha tena mchezaji aliyevunja rekodi ya usajili kwa klabu ya pauni milioni 72, Nicolas Pepe katika kikosi chao na wanataka kumuuza mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 28 msimu huu. **(Telegraph)**

### LUKAKU OFA NONO

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30 amepewa ofa ya pauni milioni 20 kwa msimu na klabu ya Al-Hilal ya Saudi Arabia. **(Guardian)**

### KONE AVUTIA EPL

KLABU za Aston Villa na Wolverhampton Wanderers zinavutiwa na kiungo wa kati wa Borussia Monchengladbach Mfaransa Manu Kone mwenye umri wa miaka 22, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Liverpool. **(Mail)**

### SPURS YAKOMAA NA RAYa

TOTTENHAM Hotspur inakaribia kuafikiana na golikipa wa Brentford, David Raya mwenye umri wa miaka 27 na wanatumai kujadili ada ya chini ya pauni milioni 40 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania. **(Standard)**

### ALBA KUMFUATA MESSI

MLINZI wa Barcelona na Hispania, Jordi Alba mwenye umri wa miaka 34, yuko kwenye mazungumzo na Inter Miami kuhusu kuhamia Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MSL. **(Fabrizio Romano)**

### BAENA ATAKIWA BARCA

BARCELONA inamfuatilia kiungo wa kati wa Villarreal, Alex Baena mwenye umri wa miaka 21 kama mbadala wa kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 32. **(ESPN)**

### HUMPHREYS AWANIWA CHELSEA

KLABU ya Coventry City inavutiwa na beki wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20, Bashir Humphreys. **(Standard)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZ… A ULAYA



# MESSI: SIFIKIRII KUCHEZA KOMBE LA DUNIA LA 2026

●●●Asema lile la nchini Qatar lilikuwa la mwisho kwake, lakini ataona mambo...

**BEIJING, China**

LIONEL Messi amethibitisha kuwa "hafikirii" kama atacheza Kombe lingine la Dunia baada ya kuiongoza Argentina kutwaa ubingwa wa mashindano hayo mwaka jana nchini Qatar.

Messi ambaye ana umri wa miaka 35 alisema hayo katika mahojiano na vyombo vya habari vya China kuhusu mustakabali wake kwenye michuano hiyo mikubwa ambayo inayofuata itafanyika mwaka 2026 kwa ushirikiano wa nchi tatu, Marekani, Canada na Mexico.

"Nimesema mara kadhaa hapo awali kwamba sifikirii hivyo, kwamba hiyo (2022) lilikuwa Kombe langu la mwisho la Dunia," alisema alipoulizwa na Titan Sports ya China kwenye mahojiano.

"Nitaona jinsi mambo yanavyokwenda, lakini kwa nadharia sidhani kama nitakuwepo kwa Kombe lijalo la Dunia," aliongeza.

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or kwa sasa yuko jijini Beijing nchini China ambako Argentina itacheza mechi ya kirafiki na Australia leo Alhamisi.

Argentina itacheza mechi hiyo ya kirafiki kwenye Uwanja wa Workers unaochukua watu 68,000 mjini Beijing.

Messi atatimiza miaka 39 wakati wa mashindano yajayo.

Messi wiki iliyopita alitangaza kujiunga na klabu ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MSL, baada ya mkataba wake wa miaka miwili na Paris Saint-Germain kukamilika. Mechi hiyo ni marudio ya mchezo wa hatua ya 16 bora kati ya timu hizo kwenye Kombe la Dunia mjini Doha, ambapo Argentina ilishinda 2-1.

Huku mashabiki wa China wakitamani kumuona nyota huyo wa zamani wa Barcelona akicheza, tiketi zimeuzwa mapema na haraka licha ya kuuzwa kwa bei ya juu hadi Yuan 4,800 (Dola 671) sawa na Sh. 1,600,335.

## HABARI MICHEZO



# RASHFORD AWAPUUZA WANAOMKOSOA ENGLAND

**LONDON, England**

MARCUS Rashford amesema amejitolea kikamilifu kwa silimia 100 kwa timu ya taifa ya England na hajali ikiwa kuna watu watamkosoa au kutilia shaka kujitolea kwake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anajiandaa kwa mechi ya kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Malta na Macedonia Kaskazini baada ya kujiondoa kwenye kikosi hicho Machi kutokana na jeraha.

Rashford amelazimika kujiondoa katika kambi nyingi hivi karibuni lakini uamuzi wake wa kwenda New York wakati England waliposhinda mechi yao ya kwanza ya Kundi C 2-1 nchini Italia ulizua mjadala.

Gareth Southgate alitetea uamuzi wa mshambuliaji huyo mwenye mataji 51 kuelekea Marekani wakati huo na fowadi huyo wa Manchester United amesema hakuona tatizo.

"Sikuona, kuwa mkweli kwako," alisema Rashford.

"Nahitaji muda wa kupona, kwa hiyo nilichukua safari fupi, siku nne, kisha nikarudi kufanya mazoezi na kujaribu tu kujiandaa haraka iwezekanavyo.

"Ukiwa na majeraha, huwezi kutabiri ni lini yatapona.

"Nashukuru nina matatizo machache ya misuli na aina ya majeraha, lakini mara kwa mara unapata majeraha. Mengi ya majeraha yangu yamekuwa hivyo."

Alipoulizwa ikiwa watu wanaohoji kujitolea kwake kwa nchi yake, Rashford alijibu: "Kusema kweli, sivyo wanavyofikiri.

"Ninajua kuwa nimejitolea kwa asilimia 100, watu watasema kile watakachosema, hainisumbui sana."

England inajianda kucheza mechi ya kufuzu Euro 2024 dhidi ya Malta kesho Ijumaa kabla ya kuwavaa Macedonia Kaskazini Jumatatu

# Brazil, Hispania kupinga ubaguzi wa Vinicius Jr

**MADRID, Hispania**

BRAZIL itacheza na Hispania katika mechi ya kirafiki Machi mwakani kama sehemu ya kampeni ya kupinga ubaguzi wa rangi kumuunga mkono Vinicius Jr.

Mchezo huo utapigwa kwenye Uwanja wa Bernabeu jijini Madrid nyumbani kwa winga wa Brazil Vinicius katika klabu ya Real Madrid.

Vinicius alilengwa kwa unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi mara kadhaa nchini Hispania alipokuwa akiichezea Real katika kampeni zilizopita.

"Hakuna nafasi ya matusi ya kibaguzi katika soka letu," alisema rais wa Chama cha Soka cha Hispania, Luis Rubiales.

Rubiales na mwenzake wa FA (CBF) wa Brazil Ednaldo Rodrigues walizindua kampeni yao ya kupinga ubaguzi



wa rangi chini ya kauli mbiu "Ngozi moja".

"Ni muhimu kuelewa kwamba adhabu kali zaidi inapaswa kutumika katika kesi za ubaguzi wa rangi na mamlaka ya soka," alisema Rodrigues.

"Faini haitoshi. Klabu zinahitaji kuwajibika pia.

"CBF lilikuwa shirikisho la kwanza la soka kupitisha vikwazo vikali zaidi kwa kesi za ubaguzi wa rangi, kama vile kukatwa kwa pointi katika msimamo wa ligi, kufungwa kwa viwanja au kufungiwa kwa mashabiki na wanachama wa klabu maisha yao yote.

"Tunahitaji kuongoza kampeni duniani kote kupigana na virusi hivi ambavyo vinaaibisha kila mtu katika soka."

Brazil itacheza na Guinea huko Barcelona Jumamosi na Senegal huko Lisbon siku tatu baadaye.

Tukio la hivi punde zaidi la Vinicius kudhalilishwa kwa ubaguzi wa rangi nchini Hispania lilikuja wakati Real Madrid ilipocheza na Valencia Mei.

Vinicius, ambaye kadi yake nyekundu kwa kufanya vurugu mwishoni mwa mechi ilifutwa, baadaye alisema ligi ya Hispania "ni ya wabaguzi".

# Lukaku apewa ofa nono Saudi Arabia

**RIYADH, Saudi Arabia**

ROMELU Lukaku anatarajiwa kupewa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni 43 kutoka kwa miamba ya Saudi Arabia, Al-Hilal msimu huu wa joto, kwa mujibu wa ripoti.

Iwapo ofa hiyo itakubaliwa, hatua hiyo itamfanya Lukaku kuwa nyota wa hivi karibuni zaidi kujiunga na Ligi Kuu ya Saudi Arabia (Saudi Pro League) tangu fowadi Cristiano Ronaldo, ambaye alishirikiana na Al-Nassr kufuatia kuondoka kwake Manchester United Desemba mwaka jana.

Muda wa mkopo wa Mbelgiji huyo katika timu iliyomaliza nafasi ya pili kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya, Inter Milan, utafikia tamati msimu huu wa joto, huku Lukaku akitarajiwa kuungana tena na Chelsea chini ya kocha mkuu mpya Mauricio Pochettino.

Mshambuliaji huyo aliondoka Stamford Bridge chini ya hali mbaya baada ya kuwaambia kwamba angependa kuondoka kwa zaidi ya miezi sita baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 98 kwenda London Magharibi mnamo Agosti 2021.

Inasemekana kwamba Lukaku alikutana na maofisa wa Al-Hilal kujadili mkataba huo nchini Saudi Arabia siku ya Jumatatu, ingawa inaaminika kuwa atalipa kisogo soka la Ulaya kwa ofa nono zaidi.

Kwa mujibu wa Goal.com, Chelsea wako tayari kuachana na Lukaku lakini wanataka ada ya uhamisho ya zaidi ya pauni milioni 43, chini ya nusu ya ile waliyolipa misimu miwili iliyopita.

Ripoti hiyo imedai kuwa Al-Hilal wanasita kulipa bei inayotakiwa na The Blues hao na watajadiliana na mwenyekiti wa Chelsea, Todd Boehy katika jitihada za kupunguza ada hiyo.

Vinara hao wa Stamford Bridge wanajiandaa kukifanyia marekebisho kikosi chao kabla ya msimu ujao kufuatia kampeni mbaya, baada ya kumaliza katika nafasi ya 12 kwenye Ligi Kuu ya England na kushindwa kufuzu kwa michuano ya Ulaya.

Ronaldo alifungua kinyang'anyiro cha nyota wa Ulaya kujiunga na ligi ya Saudi Pro League, akikubali dili nono lenye thamani ya pauni milioni 173 kwa mwaka na Al-Nassr Januari mwaka huu.

Karim Benzema alikatisha maisha yake ya miaka 14 katika klabu ya Real Madrid ili kusaini mkataba wa pauni milioni 86 kwa mwaka na mabingwa wa Saudia Al-Ittihad, na kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante yuko tayari kusaini mkataba na klabu hiyo.

# OJWEKE AIBUKA MSHINDI WA GARI KAMPENI YA CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

JARED Ojweke ameibuka mshindi wa gari aina ya Toyota Crown katika awamu ya pili ya kampeni ya Benki ni Simbanking inayoendeshwa na Benki ya CRDB.

Akieleza namna alivyoshinda gari hilo, Ojweke alisema muamala wa mwisho alioufanya kwa kutumia programu ya Simbanking ni kutuma fedha kwa mtu aliyemwomba msaada kutokana na changamoto alizonazo.

"Kuna mama mmoja alinitumia ujumbe mfupi wa simu akiniomba msaada. Yeye ni mjane, alinieleza walilala bila kula na wameamka hawana uhakika wa chakula.

"Nilimtumia hela kidogo kupitia Simbanking. Muda mfupi baada ya kumtumia hela hiyo, ndipo nikapokea simu kutoka Benki ya CRDB wakinieleza nimeshinda gari kutokana na matumizi ya Simbanking. Nilistaajabu ila nilifurahi pia," alisema.

Ojweke alisema amekuwa akitumia programu ya Simbanking kwa muda mrefu kwa kuwa ni rahisi na ina ufanisi mkubwa tofauti na programu za benki nyingine.

"Ninamshukuru mwajiri wangu, anayenilipa mshahara ulioniwezesha kupata zawadi hii. Kwa wateja wenzangu wa Benki ya CRDB, tumieni Simbanking ili mshinde fedha taslimu, simu za mkononi hata gari kama nilivyoshinda mimi. Kuna gari kubwa la Vanguard, msipoitumia fursa, ninaweza nikashinda tena," alisema Ojweke.

Mshindi huyo ambaye amekuwa mteja wa Benki ya CRDB tangu mwaka 2001, alikabidhiwa gari hilo lenye thamani ya Sh. milioni 20 lililokatiwa bima kubwa na kujaziwa mafuta 'full tank'.

Akikabidhi zawadi hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia yameulazimu ulimwengu kuhamia katika uchumi wa kidijiti, hivyo Tanzania nayo haipaswi kubaki nyuma ndio maana wanahamasisha matumizi ya Simbanking, jukwaa lililoboresha linalokidhi mahitaji ya mteja kwa wakati.

"Leo tunamtangaza kaka yangu Jared kuwa mshindi wa gari. Yeye ni mshindi wa pili baada ya Mayani Hassan wa mkoani Dodoma kushinda miezi miwili iliyopita. Simbanking ni ya kila mtu, unaweza kumaliza mahitaji yako ukiwa mahali popote," alisema Adili.

Ikiwa benki kiongozi nchini, Adili alisema Benki ya CRDB inahakikisha wakati wote inaboresha huduma zake ili kukidhi mahitaji ya wateja ikitambua kwamba matarajio yao yanabadilika kila siku.

Balozi wa Simbanking, Priva Shayo, maarufu Privaldinho, alisema kwa maisha ya sasa gari ni nyenzo muhimu ya kurahisisha shughuli za mtu hasa mjini ambako watu wanakimbizana na ratiba.

"Kama lilivyo gari, huduma za Simbanking nazo ni muhimu kwani unaweza kununua muda wa maongezi, kununua luku au kulipia bili za maji na huduma nyingine. Mshindi wa leo anakuwa amekamilisha mahitaji muhimu kwa maisha ya mjini, watoto wake hata ndugu na marafiki nao watahamasika kutumia huduma za Simbanking," alisema Privaldinho ambaye pia ni Meneja Mawasiliano wa Klabu ya Yanga.

Kampeni ya Benki ni SimBanking ilizinduliwa mapema Februari na itadumu mpaka Desemba na kumpa kila amteja anayefanya miamala kwa Simbanking kushinda moja kati ya zawadi zinazoendelea kutolewa kila siku kabla mshindi wa jumla atakayeondoka na gari aina ya Vanguard hajahitimisha mchuano huo.

Katika kipindi cha kampeni hii, matumizi ya huduma za Simbanking sambamba na idadi ya wateja wanaojisajili katika jukwaa hili la kidijiti yameongezeka na mpaka Desemba kutakuwa na namba kubwa zaidi.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili (kushoto) akimkabidhi Jared Awando Ojweke ufunguo/namba za usajili wa gari aina ya Toyota Crown, baada ya kuibuka mshindi wa kampeni ya Benki ni Simbanking. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jogging Dar wapata elimu rushwa ya ngono

**Na Sabato Kasika**

MAKUNDI ya jogging zaidi ya 40 kutoka maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam yamepata elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono na kutakiwa kujiepusha nayo.

Aidha, yamekumbushwa kutambua kuwa rushwa hiyo ni ukatili wa kijinsia ambao umekuwa ukifanyika majumbani, mitaani na hata katika michezo ukiwamo wa jogging kwa kuwa unahusisha jinsi zote.

Baadhi ya makundi hayo ya jogging ni Safari Salama, Vegas, Mwananyamala, Umoja, Temeke, Buguruni, Serengeti, Kistone, Kopa, Big Star, Msufini, Namanga, Smart, Biafra na New Star.

Mengine ni Big Family, Physical, Fanja, Kisiwani, Kawe na Mzimuni, ambayo yote yalishiriki mbio za kilomita sita kutoka Mwananyamala na kuzunguka hadi Tandale na kurudi Mwananyamala.

Akitoa elimu hiyo katika viwanja wa Vegas Mwananyamala juzi, Mkurugenzi wa shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, alisema rushwa ya ngono imesambaa kila mahali hadi katika makundi ya jogging.

"WAJIKI tunataka vijana wote washiriki katika michezo wawe salama, kutokana na ukweli kwamba, mbali na rushwa ya ngono, kuna vitendo vya ulawiti ambavyo wanafanyiwa vijana wadogo," alisema Janeth.

Mkurugenzi huyo alisema vitendo hivyo vina madhara kiafya, kisaikolojia na kwamba ni vyema vijana wakatambua na kuviepuka, ili kuwa na taifa lenye jamii ilio na afya bora na pia maadili mema.

"Tunaendesha kampeni iitwayo 'Unga Tela Vunja Ukimya, Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana. Women Fund Tanzania (WFT), wanatufadhili kufanikisha elimu hii," alisema.

Mwenyekiti wa vilabu 10 vya jogging Kinondoni, Fatuma Dole, amesema michezo inasaidia kupunguza vitendo vya ukatili, na kwamba katika jogging wamekuwa wakiwafundisha vijana mambo mengi kuhusu maadili mema, na kufanfanua kuwa ujio wa WAJIKI ni mwendelezo wa kufanikisha vita dhidi ya rushwa ya ngono.

## Simba, Azam wapimana nguvu kwa Bajana

INATOKA UK. 24

Kuu salama bila ya majeruhi yoyote makubwa na kuhakikisha wamepata nafasi ya kufuzu kucheza kombe la Shirikisho na sasa wanahitaji kuboresha kikosi chao.

Na katika hilo, Popat alisema kuwa kwa sasa wanalazimika kuwabakiza baadhi ya wachezaji wao ambao mikataba yao ipo ukingoni akiwemo Bajana.

"Msimu ujao tunaenda kucheza kimataifa, tumeanza usajili wa nyota wa ndani kwa kumchukuwa Feisal Salum 'Fei Toto', tutasajili kulingana na mahitaji ya kikosi chetu na kuhusu Bajana haendi popote kwani tutakutana naye na kuzungumza nae kuhusu kumuongezea mkataba mwingine," alisema Mtendaji huyo.

Alisema wamedhamiria kuboresha kikosi chao na kuhakikisha wanafanya usajili wa wachezaji bora na kuwaongeza mikataba nyota wale wako kwenye mipango ya timu yao kwa msimu ujao.

## Nabi ataja maeneo ya mabadiliko Yanga SC

INATOKA UK. 24

sha wanatetea mataji yao hayo kwa kuliongezea nguvu benchi lao la ufundi kwa kuleta wataalamu ambao wataongeza ladha ya mpira zaidi kuliko walioucheza msimu huu.

Alisema usajili wa wachezaji walianza kufanya mapema wakati Ligi Kuu Tanzania ikiwa inaendelea, hivyo wanasubiri dirisha la usajili lifunguliwe ili wakamilishe taratibu zilizobakia.

"Usajili tuliufanya mapema kwa kutafuta wachezaji ambao tunawahitaji na tutakaoendelea nao msimu ujao kwa lengo la kuiboresha timu yetu."

Alisema anawashukuru mashabiki wao kutokana na ushirikiano mkubwa waliowaonesha msimu huu na kuwaahidi kuwa watahakikisha wanatafuta idadi kubwa ya wadhamini ambao watafanya Yanga ifanye vizuri zaidi.

Yanga imemaliza msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022-2023 ikiwa na pointi 78 na bingwa wa Kombe la FA na washindi wa pili Kombe la Shirikisho Afrika, CAF.

# Michezo

Alhamisi Juni 15, 2023

Nipashe




Messi: Sifikirii kucheza kombe la dunia la 2026 UKURASA 21

# NABI ATAJA MAENEO YA MABADILIKO YANGA SC

●●●Abainisha nafasi tatu zenye uhitaji muhimu zaidi, pengo la Fei Toto nalo...



**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi hatafanya mabadiliko makubwa ya usajili ndani ya kikosi hicho kwa ajili ya msimu ujao, lakini ataboresha baadhi ya nafasi ikiwemo safu ya kiungo, winga na ushambuliaji.

Miongoni mwa wachezaji wanaohusishwa kuwaniwa ni pamoja na Fabrice Ngoma ambaye inadaiwa kwamba, ameshakubaliana na Yanga kusaini mkataba wa miaka miwili.

Akizungumza na Nipashe, Nabi alisema amependekeza kufanya maboresho machache ndani ya kikosi cha timu hiyo kulingana na mahitaji ya msimu ujao wa mashindano.

Alisema katika nafasi ambazo anazihitaji ni kupata winga, kiungo ambaye atakuwa mbadala wa Feisal Salum 'Fei Toto', ambaye hatakuwa sehemu ya kikosi cha timu yake kwa msimu ujao baada ya kutimkia Azam FC.

"Tunahitaji kupata wachezaji watakaotutoa hapa tulipo na kutufikisha hatua inayofuata, nyota waliopo ni wazuri, lakini tunahitaji kufanya maboresho kidogo ikiwemo sehemu ya kiungo kwa kumpa mbadala wa Fei Toto, kwani endapo Khalid Aucho atakosekana, basi kuwe na mbadala wake," alisema Nabi.

Aliongeza: "Usajili wangu utakuwa na baadhi ya maingizo mapya katika kikosi changu, nitasajili mabeki wa pembeni, mawinga na washambuliaji kila sehemu wachezaji wawili."

Alisema kulingana na msimu huu wa usajili wanahitaji kuboresha baadhi ya nafasi hizo kulingana na mahitaji ya kikosi chao kwa msimu ujao ili waweze kufanya vizuri zaidi kwenye michuano ya Afrika na ikiwezekana kutwaa ubingwa.

"Tumekuwa na msimu mzuri, kufika fainali ya CAF sio jambo dogo, lakini lazima tuangalie namna ya kuboresha zaidi kikosi chetu, tayari nina ripoti mkononi, hivyo mapendekezo yangu yote yapo humo," alisema Nabi ambaye ameripotiwa kuwa kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba wake na Klabu hiyo ya Jangwani baada ya ule wa mwanzo kufikia ukingoni.

Naye Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji alisema baada ya kushika nafasi ya pili kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, wanaelekeza nguvu katika mashindano ya Ligi ya mabingwa Afrika.

"Tulicheza Fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF) kwa mara ya kwanza sasa tunakwenda kuacha alama nyingine kwenye mashindano ya Kombe la Ligi ya mabingwa Afrika," alisema Haji.

Haji aliongeza kusema kuwa wanashukuru kumaliza salama msimu huu wakiwa wametimiza malengo yao ya kuchukua makombe mawili ya Ligi Kuu na FA na kuahidi kufika mbali zaidi msimu ujao.

Alisema msimu ujao watahakiki-

INAENDELEA UK. 23

## Simba, Azam wapimana nguvu kwa Bajana

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Azam FC, Sospeter Bajana ambaye anatajwa kuwaniwa na Simba amesema kwamba yupo kwenye mazungumzo na timu zote mbili na anachoangalia ni maslahi zaidi.

Akizungumza na Nipashe, Bajana alisema bado hajafikia maamuzi ya wapi atacheza msimu ujao, na ni kweli kwamba klabu zote mbili zipo kwenye mazungumzo nae na anachoangalia zaidi ni maslahi.

"Sasa ni mapema kusema msimu ujao nitacheza wapi, kwa sababu mkataba wangu kwa sasa upo ukiongoni, nafanya mazungumzo na Azam FC kwa mkataba mpya, lakini Simba wameonesha nia, naangalia maslahi zaidi kwa sababu nina familia ambayo inanitegemea," alisema Bajana.



Hata hivyo, uongozi wa matajiri Azam umewaka wazi kuwa utahakikisha wanafanikiwa kumbakiza mchezaji huyo kwa kumuwekea dau nono.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema wanashukuru Mungu kumaliza Ligi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >